# Nipashe

Jumanne Januari 26, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580472

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11

**WAZIRI** ashtukia ufisadi, aweka ndani maofisa 4

UKURASA 5



**RIPOTI MAALUM**

**ONGEZEKO** la watu linavyotishia uhai Hifadhi ya Ngorongoro

UKURASA 4

# Hoja 9 za watumishi kudai haki serikalini

UKURASA 2



UKURASA WA 8

## OFISA UTUMISHI, WALIMU KORTINI MADAI YA RUSHWA

OFISA Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita na walimu watatu wa shule za msingi wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita wakishtakiwa...

UKURASA WA 5

## WAZIRI AAGIZA MKANDARASI KUSWEKWA NDANI SAA 17

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ametoa amri ya kuwekwa ndani saa 17 mkandarasi na wasimamizi wa mradi wa ujenzi wa majengo matano mapya katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa, baada ya kushindwa kutekeleza maagizo yaliyotolewa awali...



Rais Dk. John Magufuli akimpokea Rais wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Geita mjini Chato jana, kwa ziara ya kikazi ya siku moja. **PICHA: IKULU**

## Wadaiwa sugu ardhi kufutiwa umiliki

UKURASA 2

# JPM kuwaachia wahamiaji haramu 1,789 wa Ethiopia

UKURASA 3

**MICHEZO** DIDIER ATAMALIZA WATUKUTU NIDHAMU SIMBA - HITIMANA UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Watumishi wawasilisha hoja tisa za kudai haki serikalini

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), kimewasilisha kwa serikali hoja tisa ambazo zimekuwa kikwazo kwa watumishi wa elimu ya juu nchini, huku kikitoa mapendekezo mbalimbali.

Miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu sura ya 178 ambayo ni tatizo katika ukusanyaji na urejeshwaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika.

Akizungumzia hoja hizo zilizowasilishwa kwa Waziri Mkuu, Mwenyekiti wa THTU Taifa, Dk. Paul Loisulie, alisema kumewapo na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi kuhusu kubambikiwa madeni wasiyostahili kutokana na mabadiliko ya sheria hiyo.

Alisema katika sheria hiyo ya bodi kuna sharti la kuanza kulipa deni baada ya zaidi ya miaka miwili baada ya kumaliza au kusitisha masomo hali inayosababisha wanufaika kuandamwa na malipo ya adhabu mbali na asilimia 15 ya makato ya mshahara wakati wa marejesho yao.

"Mwanzoni sheria iliweka angalizo kuwa makato ya mkopo kwenye mshahara wa mfanyakazi mnufaika yasizidi theluthi moja ya mshahara, lakini marekebisho haya hayajazingatia umuhimu huu wa kiwango cha makato na kushusha morali ya kufanya kazi," alisema.

Hata hivyo, alisema utaratibu ulioanzishwa na Bodi hiyo wa tozo ya kutunza thamani (VRF) umeonyesha mdaiwa atalazimika kulipa deni kwa muda mrefu na kushindwa kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

Alisema chama hicho kinashauri serikali kufanyia marekebisho mbalimbali sheria hiyo ikiwamo kupunguza makato ya asilimia 15 ili kuwapunguzia machungu wafanyakazi.

**MASLAHI YA WAFANYAKAZI**

Alisema licha ya serikali kulifanyia kazi kwa kiwango kikubwa suala la malimbikizo ya mishahara, lakini bado wafanyakazi wana madai mengi.

"Tunashauri serikali kuendelea kujipanga kulipa madeni yote halali yanayowasilishwa na vyuo vijitahidi kuzuia madeni mapya kuzalishwa," alisema.

**UPANDISHAJI VYEO**

Dk. Loisulie alisema kumekuwapo na mkanganyiko usio wa lazima katika utekelezaji wa nyaraka za upandishaji vyeo hali inayosababisha kuchelewa kupata mishahara mipya inayoendana na vyeo vyao.

"Tunashauri Ofisi ya Rais, Utumishi iendelee kutoa nyaraka za kutoa ufafanuzi kwenye taasisi za umma ili kuepuka tafsiri tofauti kwa taasisi moja hadi nyingine," alisema.

**MABADILIKO YA SHERIA YA UTUMISHI**

Alisema marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma namba nane ya mwaka 2002 yaliyofanywa mwaka 2016 yamesababisha kero kubwa kwa watumishi hasa utaratibu wa kushughulikia masuala ya kinidhamu katika utumishi wa umma.

Alisema THTU inashauri serikali kuifanyia marekebisho sheria katika Sura ya 298 kwa kuondoa sharti la lazima kwa mtumishi wa umma kumaliza kwanza nafuu zote za kisheria zinazoainishwa kwenye sheria ya utumishi wa umma kabla ya kutafuta nafuu za kisheria kwenye sheria ya kazi.

**BIMA YA AFYA**

Alisema hivi karibuni kumetokea mabadiliko katika utoaji wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) hali ambayo inaathiri wafanyakazi wote nchini ikiwamo mabadiliko ya wategemezi.

"Kumwondoa mtoto ambaye ametimiza miaka 18 kwenye utegemezi licha ya kuwa bado yupo chini ya wazazi, kwa mazingira ya kitanzania watoto hawa bado ni wategemezi kwa kuwa wapo masomoni, hii hali imeongeza mzigo kwa wazazi kulipa Sh. 50,400 anapokwenda chuoni," alisema.

Alishauri mfuko huo kuruhusu utaratibu uliokuwapo awali wa kuendelea kuwepo kwa wategemezi vijana hao hadi atakapofikisha miaka 26.

Pia, alishauri endapo kuna utofauti wa kadi na huduma zinazotolewa mfuko unatakiwa kuwa wazi ili kutoibua malalamiko.

**MABORESHO YA MIUNDO YA UTUMISHI**

Alisema THTU inaamini kuwapo kwa miundo inayofanana ya taasisi hizo kutapunguza kila taasisi kuwa na muundo wake na kupunguza kuhama kwa sababu za mishahara.

**UTAWALA BORA**

Alisema baadhi ya viongozi wa taasisi hizo wamekuwa wakikiuka misingi ya utawala bora kwa sababu zisizoeleweka ikiwamo kuficha nyaraka zinazotoka serikalini zinazohusu maslahi ya wafanyakazi.

Aliomba serikali kuzielekeza menejimenti za taasisi za elimu ya juu kuzingatia miiko ya utawala bora wakati wa utekelezaji wa mamlaka yao.

**KILIO VYUO BINAFSI**

Dk. Loisulie alisema wafanyakazi waliopo vyuo binafsi wanakabiliwa na tatizo la kutolipwa mishahara kwa wakati, waajiri kutowasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na bodi ya mikopo.

"Tunashauri serikali kuzihamasisha na kushauri taasisi binafsi za elimu ya juu kubuni vitega uchumi vya kuongeza pato la taasisi ili kuepukana na kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi," alisema.

Alisema wanaamini serikali itachukua hoja hizo na kuzitafutia ufumbuzi ili kuwa na tija kwa wafanyakazi.



Baadhi ya wamachinga wakiendelea na shughuli zao eneo la Mbezi Luis jijini Dar es Salaam juzi, huku Manispaa ya Ubungo ikiendelea na maandalizi ya kuhamisha wafanyabiashara wote wa eneo hilo na kuwapeleka kwenye masoko rasmi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wadaiwa sugu ardhi kufutiwa umiliki

**Na Munir Shemweta**, SIMIYU

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewaagiza maofisa ardhi katika halmashauri nchini kuanza kuwafutia umiliki wa ardhi wadaiwa wote sugu wa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria.

Mmiliki yeyote wa ardhi anapaswa kulipa kodi ya pango la ardhi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa masharti ya umiliki kwa mujibu wa kifungu 33 (1) cha Sheria ya Ardhi Na 4 ya mwaka 1999.

Pia kifungu cha 48(1) (g) kinaelekeza kuwa kodi ya ardhi isipolipwa kwa kipindi cha miezi sita baada ya mmiliki kutumiwa ilani ya madai, mmiliki huyo anaweza kufutiwa milki yake.

Akiwa katika ziara ya siku moja katika Mkoa wa Simiyu, Januari 25, kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi na kuzungunza na watendaji wa sekta ya ardhi, Naibu Waziri wa Ardhi aliwaelekeza wataalamu wa sekta ya ardhi kuhakikisha wanatekeleza matakwa hayo ya kisheria Na 4 ya mwaka 1999 kwa kuisimamia vyema.

"Nawaagiza maofisa ardhi katika halmashauri zote kuhakikisha sheria inachukua mkondo wake na msiendelee kuwalea wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi na mzingatie sheria Na. 4 ya ardhi wakati mnatekeleza majukumu yenu ikiwamo kufuta umiliki baada ya miezi sita kwa wadaiwa," alisema.

Aliwataka wenyeviti wa mabaraza ya ardhi ya nyumba na wilaya kutekeleza majukumu yao kwa kusaidia kuharakisha usikilizaji mashauri ya wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi ili kutoa haki kwa haraka.

"Hatuhitaji watu wapelekwe kwenye mabaraza ya ardhi ya nyumba na wilaya halafu mashauri yakae huko kwa miaka mitano tunataka mashauri yaishe haraka kwa mujibu wa sheria," alisema.

Vile vile, amewataka wakurugenzi katika halmashauri za Mkoa wa Simiyu kuzitumia vyema idara za ardhi katika masuala yote yanayohusu ardhi ikiwamo upangaji wa miji.

Alisema mamlaka za upangaji miji ziko chini ya halmashauri hizo na kusisitiza kuwa wakurugenzi hao wasipozitumia vyema kuna hatari ya kuendelea kwa ujenzi holela.

Pia Dk. Mabula ameonyesha kutoridhishwa na kasi ndogo ya ukusanyaji kodi ya pango la ardhi katika Mkoa wa Simiyu kwa kukusanya Sh. 87,654,120 sawa na asilimia 24, huku mkoa ukidai zaidi ya Sh. bilioni 5.5 kutoka kwa wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi.

Kwa upande wake Kamishna Msaidizi wa Ardhi katika mkoa huo, Simiyu Mwakatumbula, alimweleza Dk. Mabula kuwa ofisi yake itahakikisha inaongeza kasi ya kufuatilia wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi ili iweze kukusanya madeni na kufikia malengo ya makusanyo ya kodi iliyojiwekea.

Hata hivyo, alisema pamoja na jitihada za mkoa kuhakikisha wadaiwa wote wa kodi ya ardhi wanalipa, kuna changamoto kwa baadhi ya taasisi kutoonyesha jitihada zozote za kulipa na kutolea mfano wa VETA, SIDO na SHIRECU.

HABARI KITAIFA

# JPM kuwaachia wahamiaji haramu 1,789 wa Ethiopia

Na Elizabeth Zaya

SERIKALI ya Tanzania imesema iko tayari kuwaachi huru wahamiaji haramu 1,789 ambao wamefungwa kwa makosa ya kuingia nchini bila vibali.

Akizungumza wakati akimkaribisha Rais wa Ethiopia, Zahle Zewde ambaye alitembelea nchini jana kwa ziara ya kikazi ya siku moja, na kufanya mazungumzo Chato mkoani Geita, Rais John Magufuli alisema wako tayari kuwasamehe na kuwarudisha kwao wahamiaji hao haramu bila masharti yoyote.

"Kuna wafungwa 1,789 kutoka Ethiopia ambao ni wale wanaoingia nchini isivyo halali na wamehukumiwa.

Tumezungumza namna ya kupanga mbinu za kuwaruhusu warudi kwao na nimemweleza kwamba hatuna masharti na tunawaruhusu waondoke free (huru)," alisema Rais Magufuli.

"Hao wakimbizi ambao wengine wamekaa zaidi ya miaka saba watarudi kwao na niko tayari kuwaachi hata wale ambao watakuwa wamefungwa leo (jana), ili waondoke, huo ndio undugu."

Katika mazungumzo yao, viongozi hao walikubaliana mambo mbalimbali ikiwamo kuimarisha uchumi kati ya nchi hizo mbili.

Pia kuimarisha ushirikiano katika majeshi, huku Tanzania ikiahidi kupeleka walimu wa kufundisha lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Adis Ababa nchini Ethiopia.

Makubaliano mengine ni kuimarisha sekta ya mifugo, huku Tanzania ikiomba kujifunza kwa nchi hiyo ambayo inafanya vizuri na kufaidika na mifugo yake.

"Ethiopia ni ya kwanza kwa mifugo Afrika, sisi ni wa pili, lakini yenyewe imefaidika, inatengeneza bidhaa ambazo inaziuza hadi Ulaya, lakini Tanzania bado hatujafaidika, tumewaomba tujifunze kwao, kwa kukaribisha uwekezaji ili tuone namna ya kuendeleza sekta ya mifugo," alisema Rais Magufuli.

Jambo jingine ambalo walikubaliana ni kuanzisha vikao vya mazungumzo vya kuimarisha ushirikiano kati ya pande hizo ambavyo wamewaagiza mawaziri husika kushughulikia hilo ili vianze kati ya Machi na Aprili mwaka huu.

Pia Rais Magufuli alisema wameiomba nchi hiyo kuirejeshea Tanzania ardhi ambayo ilinyang`anywa baada ya kushindwa kuiendeleza kwa ajili ya kujenga ubalozi nchini humo, huku Tanzania nayo ikisema tayari imetoa hekta tano za ardhi kwa Ethiopia kwa ajili ya kuendeleza ubalozi wao jijini Dodoma.

"Ethiopia iko juu sana kiuchumi Afrika, na kama sikosei mpaka mwaka jana ulikuwa unakuwa kwa asilimia tisa, kwa hiyo kuna haja kuendeleza uhusiano uliopo ili pande zote zinufaike kiuchumi," alisema Rais Magufuli.

"Tanzania na Ethiopia zina uhusiano mzuri tangu kuanzishwa kwa Umoja nchi za Afrika na harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na tumeendelea na uhusiano haya ambayo yamenufaisha nchi zetu."

Rais Magufuli alisema katika miaka ya hivi karibuni ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi hizo umeimarika.

"Kwenye miaka ya hivi karibuni ushirikiano wa kibiashara umeimarika, mwaka 2016 ulikuwa Sh. bilioni 3.07 na mwaka 2019/2020 umefikia Sh. bilioni 13.55, na kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimesajili miradi 13 kutoka Ethiopia yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 14.57 ambazo zimetoa ajira 677,"alisema Rais Magufuli.

Sekta nyingine ambayo alisema wamekuwa wakishirikiana ni katika usafiri wa anga na utalii na kwamba Bodi ya Utalii nchini (TTB) na Shirika la Ndege la Ethiopia zimeingia makubaliano ya matangazo ambayo yamesaidia kuongeza idadi ya watalii Tanzania.

"Tumeshirikiana katika sekta ya usafiri wa anga na utalii, Shirika la Ndege la Ethiopia limekuwa likifanya safari zake katika viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema Tanzania pia imekuwa ikipata fursa ya masomo katika nyanja za marubani na wahandisi wa ndege na kwamba mpaka sasa marubani 75 na wahandisi wa ndege 20 wamepata masomo nchini humo.

Kwa upande wake Rais huyo wa Ethiopia, alisema nchi yake iko tayari kuongeza ushirikiano ili kukuza zaidi uchumi katika nchi hizo.

"Tutajitahidi kufanya mikutano kwa kuanza katika kipindi ambacho tumekubaliana ili ushirikiano tunaotaka ambao una mizizi imara katika nchi ya Tanzania uendelee," alisema Rais Zewde.

Pia alisema wako tayari kuanza kupitia makubaliano ya mikataba yote waliyoifanya katika nchi hizo mbili na kuangalia maeneo mengine mapya ya ushirikiano.

"Tunaona kwamba kuna eneo ambalo liko wazi kwa ajili ya kulijaza hususani katika uwekezaji, tumekubaliana biashara na uwekezaji kwa sababu tunaona kwamba nchi za Afrika lazima ziwekeze Afrika," alisema Zewde.

Na eneo la mifugo ni la kipaumbele zaidi kwa uwekezaji kwa sababu nchi hizo zinaongoza katika sekta hii."

Kuhusu suala la kujipanga kuja kuwachukua wahamiaji hao haramu, Rais Zewde aliishukuru serikali ya Tanzania kwa kuwaachia bila masharti na kwamba watafanya kila njia kuja kuwachukua.

Pia aliishukuru Tanzania kwa kuwapatia walimu wa Kiswahili na kwamba wako tayari kuwapokea.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

TRAINING INSTITUTE

KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW).

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Institute ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 01/03/2021. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) terminal one kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04/02/2021.

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini kidato cha nne na ufaulu mzuri hasa masomo ya kiingereza, Jiografia na Historia
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini.

Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.
i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae -CV

**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Institute**
**Box no 543**
**Dar**
**Email , training@airtanzania.co.tz**

**Mob: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING INSTITUTE.**



PC Box 123456 | Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +254 20 123456 | Fax: +254 20 123456 | email: info@airtanzania.com | website: www.airtanzania.com

NHC
TUNAJENGA TAIFA LETU

**TAARIFA KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA NHC WANAODAIWA KODI NA MALIMBIKIZO**

1. Shirika la Nyumba la Taifa linawashukuru wapangaji wake walioweza kulipa kodi na malimbikizo yao baada ya kupewa notisi ya siku kumi na nne (14) ya kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa. Aidha, wapo wapangaji wachache ambao bado wanadaiwa kodi na malimbikizo hadi sasa.

2. Kwa mara nyingine, Shirika linatoa siku thelathini(30) kwa wapangaji wanaodaiwa kodi na malimbikizo kufika katika ofisi za Shirika zilizo karibu nao ili kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa.

3. Shirika linawashauri wapangaji wote kutumia fursa hii kulipa madeni yao na baada ya muda huu uliowekwa kukamilika, Shirika litatumia taratibu za kisheria kukusanya kodi na malimbikizo yanayodaiwa wapangaji ikiwemo kukamata na kupiga mnada mali za wapangaji ili kufidia kodi na malimbikizo yanayodaiwa. Aidha, baada ya muda huu kupita, Shirika halitasita kutangaza kwenye vyombo vya habari majina ya wadaiwa wote sugu ili umma ufahamu watu wanaokwamisha maendeleo ya Shirika na Taifa kwa kutokulipa kodi.

4. Tunashukuru wapangaji wote wanaotimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na kuliwezesha Shirika na Taifa kuwaletea maendeleo watanzania kwenye sekta ya nyumba.

**IMETOLEWA NA: OFISI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII**
**NHC-MAKAO MAKUU**

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**
**MAKAO MAKUU S.L.P 2977 | DAR ES SALAAM TANZANIA**
**| SIMU: +255 22 2105001-5 | NUKUSHI: +255 22 2105000**
**BARUA PEPE: dg@nhctz.com | TOVUTI: www.nhctz.com**

RIPOTI MAALUM

# Ongezeko la watu linavyotishia uhai Hifadhi ya Ngorongoro

## Wafikia zaidi ya asilimia 1,000



Moja ya vijiji katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), eneo ambalo lina ongezeko la watu na mifugo kiasi cha kushindwa kuwa na uwiano wa uhifadhi na shughuli za kibinadamu. **PICHA: SALOME KITOMARI, NGORONGORO**

**Na Salome Kitomari,** aliyekuwa NGORONGORO

ENEO la Hifadhi ya Ngorongoro lililoanza mwaka 1959 likiwa na watu 8,000, sasa limeelemewa kwa idadi kubwa ya watu zaidi ya 100,000, huku kukiwa na ongezeko la mifugo kiasi cha kutishia uhai wao.

Ngorongoro ilianza baada ya kumegwa kutoka eneo la Serengeti Game Reserve na kuunda Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliyo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), baada ya watu 4,000 kuhamishiwa ndani ya Ngorongoro na kuanza uhifadhi na makazi.

"Najaribu kuitazama Ngorongoro miaka 10 ijayo kwamba itakuwa katika hali gani kama kasi ya watu itakuwa hii, shughuli za uhifadhi zitakuwa ngumu, migogoro baina ya jamii na wanyama itaongezeka, tutawezaje kwenda pamoja na maendeleo endelevu ya binadamu na uhifadhi," Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Freddy Manongi, anaeleza hofu yake.

Mathalani, anasema hivi karibuni diwani mmoja alinitumia picha ya fisi aliyevamia boma na kuua kondoo 38, wananchi walipiga simu wakiomba msaada tuzuie, mambo kama hayo kujitokeza ambayo ni ngumu kuzuia kitaalamu, jambo ambalo linaonyesha kila shughuli sasa inasababisha migogoro baina ya pande mbili.

Anasema kamisheni iliyoundwa na wizara kuangalia sera ya matumizi mseto ya eneo la Ngorongoro na timu ilihoji watu wengi na kushirikisha wadau kutaka kujua hatima ya eneo hilo ambalo kwa sasa linachangamoto nyingi.

"Balance (uwiano) kati ya uhifadhi wa wanyamapori, malikale na maendeleo ya binadamu ndani ya hifadhi imefikia mahali pagumu sana, kila unachofanya kwa maana ya uhifadhi kina athari kwa maisha ya binadamu wanaoishi ndani ya hifadhi na kila ruhusa au fursa unayoitoa kwa wenyeji inaathari hasi kwa uhifadhi," anasema na kuongeza;

"Hiyo tume imeona hali hiyo wazi na kumekuwa na malalamiko mengi kwa wahifadhi kuhusu idadi ya watu, lakini uharibifu unaotokana na uhifadhi, kumekuwa na malalamiko mengi kwa jamii kuwa shughuli za uhifadhi zinawaumiza," anabainisha.

Kwa mujibu wa Dk. Manongi, Tume ilimaliza kazi Mei mwaka huu, na kuwasilisha ripoti kwa Waziri wa Maliasili na kubwa waliloshauri ni eneo hilo kugawanywa katika kanda na kila moja iwe na idadi ya shughuli za uhifadhi na kibinadamu zinazofanyika kama suluhisho.

"Hii itasaidia kutenga maisha ya binadamu na maisha ya wanyamapori, itawapata fursa kwa wenyeji kuendelea na shughuli zao kama kawaida huku uhifadhi, pia ukiendelea bila kuwa na mgongano baina ya pande mbili," anasema.

Akiwasilisha mada ya 'ilikotoka, ilipo na inakokwenda Ngorongoro', Ofisa Mwandamizi wa Uhifadhi, Dk. Elibariki Bajuta, anasema majukumu ya kisheria ya Ngorongoro ni kuendeleza uhifadhi na utalii, wenyeji waliopo ndani ya hifadhi na kwamba kidunia ni muhimu sana.

"Tukishindwa kubalance (uwiano) wa matumizi ya eneo hili ndiyo tutashindwa kufikia malengo husika," anasema.

### ONGEZEKO LA MIFUGO NA WATU

Anasema Ngorongoro ilifanya sensa kujua idadi ya mifugo, watu na makazi ndani ya eneo, ili kupanga matumizi na kuona mfumo wa matumizi ya eneo hilo kwa ushirikiano.

Kwa mujibu wa Dk. Bajuta, pamoja na mafanikio makubwa kuna tatizo kubwa la ongezeko la watu ambalo siyo wa kuzaliana bali walioingia ndani ya hifadhi.

"Miaka ya 90 aliyekuwa Waziri Mkuu, John Malecela, aliruhusu kilimo cha kujikimu ambacho kililete watu wengi sana ndani ya hifadhi, tangu kuanza kwa hifadhi mwaka 1959 kuna ongezeko la watu zaidi ya asilimia 1,000, hii si hali nzuri kwa utalii na uhifadhi," anasema.

"Mifugo nayo imeongezeka kwa kiasi kikubwa mno na asilimia 20 wanamiliki asilimia 80 ya mifugo iliyopo na kubwa zaidi kuna ongezeko kubwa la magonjwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa wanyama wanaofugwa na kutoka kwa wanyama wanaofugwa kwenda kwa wanyamapori, hadi kwa wenyeji na kuleta balaa," anasema.

"Magonjwa haya hata tiba yake ni shida sana maana jamii maisha wanayoishi siyo mazuri sana," anasema.

### UHARIBIFU WA MAZINGIRA

Dk. Bajuta anasema kasi ya uharibifu wa mazingira ni kubwa kutokana na ongezeko la watu na mifugo pamoja na wanyamapori, ushindani katika utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi, utalii na maendeleo ya watu ni changamoto.

Anasema kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na sababu nyingi kama kuongezeka kwa watu na wanyama wanaofugwa vyanzo vya maji vimepotea na kupungua kwa huduma hiyo muhimu hifadhini.

"Kubwa zaidi ni kuongezeka kwa migogoro baina ya wanyamapori na binadamu, mfano fisi kaua kondoo 38, kuna kaya zaidi ya 20,000, tuna askari pungufu 300, huwezi kulinda kila kaya na mifugo, haya yote yapo nje ya hifadhi ila ndani ya hifadhi ni ngumu sana," anasema na kuongeza:

Nje ya hifadhi tembo wanakula mazao ya wananchi na kwa sheria ya wanyamapori mamlaka hairuhusiwi kutoa kifuta machozi kwa sababu tayari tunaishi na wanyamapori.

### MAGUGU VAMIZI

"Makazi yameongezeka sana kwa sababu watu wameongezeka, bado tunajitahidi kubana kuhakikisha hawajengi bila vibali, lakini bado changamoto ni kubwa sana na kutokana na kuongezeka kwa watu na mifugo sasa hifadhi imepata magugu vamizi," anasema.

Kwa mujibu wa Bajuta, ndani ya eneo la kreta, asilimia 70 ya eneo limepata magugu vamizi kutokana na mifugo na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu.

Aidha, anasema umaskini ndani ya hifadhi ni mkubwa unaosababishwa na sheria inayosimamia eneo hilo kwa kuwa wananchi hawaruhusiwi kufanya shughuli nyingine yoyote ya kujipatia kipato zaidi ya ufugaji na wengi hawana mifugo.

### UMASKINI/ KIWANGO CHA UJINGA

"Umaskini ni mkubwa sana ndani ya hifadhi kwamba hata mtu kumudu milo mitatu kwa siku ni ngumu sana, na ndiyo maana serikali iliamua hakuna kuwapa chakula," anasema.

Anasema sensa ya mwaka 2017 iliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ilionyesha kuwa asilimia 64.5 ya wananchi hawajui kusoma na kuandika, huku kukiwa na shule 25 za msingi na mbili za sekondari.

### HATUA ZILIZOCHUKULIWA

Anasema Ngorongoro imefikia mahali wakijibana katika kusaidia jamii wanaumiza uhifadhi na wakijibana katika kulinda wananchi wanaumiza uhifadhi na ndiyo maana wamekuja na mipango mbalimbali.

Mipango hiyo ni ya kupambana na magugu vamizi inayotekelezwa chini ya Ofisi Makamu wa Rais, mwingine ni kuhakikisha utalii endelevu ndani ya hifadhi kwa kuwa kipindi cha juu cha utalii kuna magari 700 ndani ya kreta, kuboresha miradi ya maendeleo na kuboresha mifugo ili kuachana na idadi kubwa ya mifugo, hifadhi na mifugo viwepo.

"Kuna mambo hayapo ndani ya uwezo wetu kama kupitia upya muundo wa eneo la Ngorongoro, kamati imeshafanyakazi yake na kuwasilisha wizarani tunasubiri matokeo," anasema.

Pia wanafanya mapitio ya mpango mkuu wa Ngorongoro unaotarajia kukamilika hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya sheria iliyounda eneo hilo ambayo yalifanyika mara ya mwisho mwaka 2002, itayokuja na hali halisi ya hifadhi na hatua za kuchukua.

ITAENDELEA KESHO

## HABARI KITAIFA

# Naibu Waziri aagiza mkandarasi kuswekwa ndani

**Na Futuna Seleman**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ametoa amri ya kuwekwa ndani saa 17 mkandarasi na wasimamizi wa mradi wa ujenzi wa majengo matano mapya katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa, baada ya kushindwa kutekeleza maagizo yaliyotolewa awali.

Aliagiza kuwaweka ndani mmoja wa wakurugenzi wa kampuni ya CF Builders ya jijini Mwanza, Fredy Chacha na wasimamizi wa mradi huo, Mhandisi Laurent Vicent na Thobias Ntobi, wote wa kampuni hiyo iliyopewa kazi ya kujenga mradi huo baada ya kushindwa kutoa sababu zilizosababisha kutotekeleza maagizo aliyoyatoa Desemba 19, mwaka jana na mradi huo kusuasua.

Alisema mradi huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.8, ulipaswa kukamilika tangu mwaka jana, lakini mpaka sasa umetekelezwa kwa asilimia 16 pekee, huku kampuni hiyo ikiwa imeshalipwa zaidi ya asilimia 20.

Alisema Desemba 19, alitoa maagizo mbalimbali kwa kampuni hiyo ikiwamo kuhakikisha vifaa vyote vya ujenzi vinakuwa eneo la ujenzi pamoja na kuongeza watumishi wa kutosha jambo ambalo wamelikaidi.

"Kwa kuwa nilikuja hapa tarehe 19 mwezi uliopita na kuwapa maagizo ambayo naona hamjataka kuyatekeleza, sasa mtakwenda kulala ndani mpaka kesho saa nne kamili na mnapotoka ndani mtakuja moja kwa moja site kwa ajili ya kuandaa mpango wa manunuzi wa vifaa vyote vinavyohitajika na nataka niupate kimaandishi ifikapo kesho saa 10 jioni," alisisitiza.

Alimtaka mkandarasi huyo kuongeza vibarua na mafundi wanaotoka katika maeneo ya Mpwapwa na awalipe vizuri ili kuwezesha kazi hiyo kwenda kwa kasi. Kipanga alisema mradi huo ambao ulianza kutekelezwa tangu 2019 umekuwa ukisuasua bila sababu wakati fedha za kukamilisha zipo na kuwataka wataalamu wote wanaohusika na usimamizi wa mradi huo kuanza kufuatilia kwa karibu ili ikifika mwezi Juni, mwaka huu uwe umekamilika.

# Waziri ashtukia ufisadi, awaweka ndani maofisa 4

**Na Jumbe Ismailly** SINGIDA

MAOFISA wanne wa serikali wametiwa mbaroni kwa madai ya matumizi mabaya ya fedha za ujenzi wa Chuo cha Mamlaka ya Elimu ya Ufundi (VETA) wilayani Ikungi, Mkoa wa Singida.

Walitiwa mbaroni na Jeshi la Polisi kwa agizo la Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga.

Hatua hiyo ilifuatia baada ya Kipanga kuikataa taarifa ya ujenzi wa majengo ya chuo hicho kinachojengwa katika Wilaya ya Ikungi, iliyotolewa na Mkuu wa Chuo cha VETA Singida, kutokana na kutoridhishwa na thamani ya matumizi ya fedha zilizotumika.

Kutokana na kutoridhishwa na hatua yaliyofikia majengo hayo na thamani ya fedha zilizotumika, ndipo Naibu Waziri huyo aliliagiza Jeshi la Polisi kuwaweka chini ya ulinzi maofisa wanne wa serikali waliokuwa wakisimamia mradi wa ujenzi wa chuo hicho, ili kupisha uchunguzi juu ya matumizi mabaya ya fedha.

Kipanga aliagiza kukamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi kwa maofisa hao baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa majengo ya chuo hicho unaotarajia kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 1.6 kitakapokamika na kubaini kuwapo kwa dalili za ufisadi katika matumizi ya fedha hizo.

Kutokana na matumizi mabaya ya fedha yenye kutia shaka, Naibu aliivunja kamati ya kusimamia mradi huo wa ujenzi wilayani Ikungi.

Kipanga aliwataja watuhumiwa wanaoshikiliwa kwa uchunguzi ni Mkuu wa Chuo cha VETA, Paulo Batoleki, Ofisa Manunuzi, Lyina Nimrod, Msimamizi wa ujenzi wa majengo ya chuo hicho, Salumu Mohamed na Kaimu Mhasibu, Dlusy Rwejuna.

Pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Ikungi kuanza uchunguzi mara moja dhidi ya maofisa hao.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogoro, alisema tangu kuanza kwa ujenzi wa chuo hicho kumekuwapo na usiri juu ya upatikanaji wa taarifa kutoka kwa mamlaka inayosimamia shughuli hizo za ujenzi.

Alisema licha ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo kutembelea mara kadhaa kwenye shughuli za ujenzi, lakini walikuwa wakikwamishwa kupata taarifa za mikataba pamoja na gharama za mradi huo kutoka kwa wahusika.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi huo kwa Naibu Waziri, Mkuu wa Chuo cha VETA Mkoa wa Singida, Paulo Batoleki, alisema mradi huo ulioanza kutekelezwa Machi 18, mwaka jana unatarajia kukamilika katika kipindi cha miezi 12, na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.6.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, Mashaka Mgeta, akizungumza juzi kwenye maadhimisho ya miaka 100 ya kuanzishwa kwa Mahakama Kuu na kuwataka wananchi kutumia fursa hiyo, kupata huduma za kisheria na kuepuka gharama wanazoweza kutumia kwenda kwa wanasheria hasa wa kujitegemea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU** .


KCOM

TUNA AJIRI

SALES EXECUTIVE

VIGEZO VYA KAZI:

- Cheti cha Form IV
- Muajiriwa awe anaweza kuongea na kuandika Kiiengereza na Kiswahili.

WASILIANA KWA 0624279186
Email: deotrophis@gmail.com


## KUMBUKUMBU



**TAREHE 25/01/2021**

**KUMBUKUMBU YA MAREHEMU BABA YETU FAUSTINE PETER NYAKI**

Leo baba yetu umetimiza miaka 21 tangu uitwe na Bwana. Sisi familia yako Mama, watoto Wajukuu,ndugu, jamaa na marafiki hatujambo na bado tuna kukumbuka mno,na tunasema wamtumainio Bwana ni kama Mlima Sayuni ambao hautatikisika milele,kama milima inavyoizunguka yerusalemu ndivyo bwana anavyoizunguka familia yako.

***RAHA YA MILELE UMPE EE BWANA NA MWANGA WA MILELE UMWANGAZIE NA APUMZIKE KWA AMANI***

AMINA!!!!

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utalii wa fukwe ni muhimu, zirudi Maliasili na Utalii

**JUZI** Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Leila Muhamed Mussa, alitembelea vyombo vya habari vya IPP Media, na kueleza mikakati ya kukuza na kuendeleza utalii visiwani Zanzibar ambavyo uchumi wake unategemea biashara ya utalii kwa asilimia 28.

Baadhi ya mikakati ni kuibua vivutio vipya ikiwamo kuendeleza utalii wa majengo ya kale na utamaduni kwa kutumia wananchi wa eneo husika kupokea na kutembeza wageni.

Licha ya kuwapo kwa janga la virusi vya homa kali ya mapafu (corona), na kusababisha ugonjwa wa Covid-19, lakini jitihada mbalimbali zimefanyika kuhakikisha watalii wanaendelea kuja nchini na kwa sasa visiwa hivyo vinapokea watalii kutoka Ulaya Mashariki ambako hakujaathiriwa sana na corona.

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mpango huo wa kubuni, kuendeleza na kuboresha vivutio vya utalii, kwa kuwa sasa mtalii atakuwa na kila sababu ya kurudi kwa kuwa hakupata nafasi ya kuvimaliza alivyokuja nchini.

Tanzania imebarikiwa hifadhi za taifa 22, mapori ya akiba 32, mapori tengefu 18, Jumuiya ya Uhifadhi za Jamii (WMA), Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Maeneo ya mtawanyiko, shoroba za wazi, ambayo yote ni muhimu kwa uhifadhi.

Mara nyingi katika kila kivutio kuna bidhaa tofauti zinazouzwa kulingana na mahitaji ya mgeni, na sasa kumekuwa na jitihada za kuleta bidhaa mpya hasa baada ya kuwapo kwa janga la corona ili kumhakikishia mgeni furaha.

Mathalani, Ngorongoro wameanzisha utalii wa miamba na sura ya nchi ambayo mtalii anaweza kutembelea maeneo mbalimbali kwa safari za miguu, kujionea uumbaji wa miamba huku akiona wanyama.

Lakini Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), imekuja na bidhaa mpya za kucheza na samaki maalum kwa watalii ambao ni wanamichezo hupenda kumuona kwa jinsi alivyo mtundu, lakini mtalii anaweza kufanya safari ya kutembea umbali fulani na kulala kwenye mahema maalum au kwenda na kurudi.

Yote yanafanyika kama mbinu ya kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio mbalimbali nchini, lakini kuondokana na utalii wa mazoea kwamba utaenda kuona wanyama ukiwa ndani ya gari basi, lakini ikiwa mtalii atapika na kula chakula porini atajiona kaishi maisha ya tofauti na kuona kweli ametalii na kufurahia, ikiwamo kuongeza siku za kukaa nchini.


Waziri huyo alieleza kuwa Zanzibar imejipanga kuongeza vivutio vya utalii ili mtalii aweze kuwa na maeneo mengi zaidi ya kutembelea, jambo ambalo litaongeza siku za kuishi nchini na fedha atakazotumia, lakini itamlazimu kupanga safari nyingine ya kurudi kuona vile ambavyo hakuviona awali.

Katika kuongeza vivutio vya utalii hapa ndipo serikali inapaswa kuangalia kwa jicho la pekee utalii wa fukwe ambao haujatumika, mathalani Zanzibar ina fukwe nzuri, kubwa na zenye kusifiwa duniani, lakini bado hazijaendelezwa na kutumika vyema, ikiwa nguvu kubwa itawekezwa huko maana yake idadi ya vivutio itaongezeka.

Pia Tanzania kuna fukwe nzuri na kubwa kuanzia Tanga hadi Mtwara, lakini zipo chini ya Wizara ya Uvuvi, jambo ambalo linasababisha ziwe ni kwa ajili ya uvuvi pekee, lakini hazitumiki kwa ajili ya watu kutalii na kuliingizia taifa fedha za kigeni.

Unapotembelea mji wa Durban, Afrika Kusini utaona jinsi fukwe zilivyojengwa kisasa na mamia ya watalii wa ndani na nje huminika kutalii huku wengine wakifanya michezo mbalimbali ya kwenye maji kwa kutumia vifaa maalum. Kama huko imewezekana, maana yake fukwe za Tanzania zina nafasi kubwa ya kutumika kwenye utalii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Inakuwaje Watanzania kuonea haya Kiswahili

**K**ISWAHILI ni kati ya lugha zilizo maarufu duniani ikizungumzwa na watu wengi kama ilivyo kwa Kingereza, Kifaransa, Kichina na Kiarabu.

Ni lugha inayoeendelea kukua, kuzungumzwa na kutambulika duniani na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), linasema Kiswahili, kinazungumzwa na watu milioni 180 duniani kote.

Mwaka 1986, UNESCO ilipitisha azimio la Kiswahili kutumika kwenye vikao vyake, kadhalika azimio la kukitumia katika Umoja wa Afrika (AU), kama lugha ya mawasiliano lilishapitishwa miaka ya karibuni.

Kiswahili kinazungumzwa zaidi Afrika Mashariki nchini Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na pia kinatumiwa Afrika ya Kati Visiwa vya Ngazija (Comoro), Malawi, Afrika Kusini, Zimbabwe na Zambia.

Pamoja na urithi huu wa kujivunia kizazi cha sasa hawakifahamu na Watanzania wengi waliozaliwa na kukulia nchini, hukikwepa.

Leo kuna mchanganyiko wa lugha mtu akizungumza anachanganya Kiingereza na Kiswahili 'Kiswakinge au Kiswanglish', kwa tafsiri mbili au zaidi aonekana msomi au ametembelea zaidi nchi zinazozungumza Kiingereza.

Ipo dhana kuwa, mzungumzaji wa lugha ngeni ni kati ya waliokwenda shule hadi chuo kikuu au ana uelewa zaidi na kwamba licha ya Kiswahili kuhitaji kukuzwa, kuenziwa, baadhi hawajivunii na kuionea aibu lugha hiyo pale wanapotaka kufikisha ujumbe kwa jamii.

Baadhi ya wasomi na wanazuoni ndiyo zaidi wanao kionea haya, wanataka kuaminisha umma kwamba wamekwishaisahau lugha mama ambayo waliizungumza tangu wakiwa ngazi ya awali shuleni, nyumbani na hata sasa mitaani.

Kundi hili na Watanzania lina nafasi kubwa ya kuitangaza lugha hiyo na kutoa maelezo yaliyonyooka katika Kiswahili bila kujali hatua za kielimu walizofikia.

Hivi sasa kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ni fursa nyingine ya kukuza lugha hiyo kupitia majukwaa yote mtandaoni hasa ya kijamii.

Kuzungumza 'Kiswanglish' katika kadamnasi au mtandaoni kwenye kurasa za twitter au whatsapp kunaishusha hadhi lugha hiyo ilijipatia umaarufu duniani.

Kwanza kuchanganya lugha, ujumbe haufiki ipasavyo na huwachosha wasikilizaji ni vyema kuchagua kutumia lugha moja mwanzo hadi mwisho katika uwasilishaji.

Tanzania inategemewa kuwa nchi ya kwanza kukipigia debe Kiswahili, ili kizungumzwe ndani na nje ya nchi badala ya kukikoroga na kusababisha kionekane duni.

Kiswahili ambacho kiliwaunganisha Watanzania kupitia juhudi zilizofanywa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, ni vyema kukienzi ikiwa ni pamoja na kuandikwa na kukidumisha kama ilivyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, kwenye maadhimisho ya lugha hiyo yaliyoanza Januari 19 hadi 20.

Ikumbukwe kuwa kuna sababu zilizosaidia kukuza na kueneza lugha kama kupitia taasisi na sekta ya elimu, uchumi kwa njia ya wafanyabiashara pamoja na watalii.

Kumekuwa na mwingiliano wa lugha ya Kiswahili kupitia wafanyabiashara ambao wanaingia nchini, kufuata bidhaa hasa kutoka mataifa yasiyo na bandari.

Pia watalii ambao wanakuja kuzuru vivutio kama mbugani, magofu yakiwamo ya Bagamoyo na Zanzibar, michoro ya mapangoni kama ya Singida na sehemu za mambo ya kale kama Bonde la Olduvai.

Tanzania ambacho ni kitovu cha Kiswahili, inaweza kukienzi kwa kutumia vyuo vikuu kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chenye Taasisi ya Utafiti wa Kiswahili (TATAKI).

NI eneo linalosomesha wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali wanaokuja nchini kujifunza lugha hiyo na kuitangaza sehemu mbalimbali duniani kwa ufasaha zaidi lakini pia inaweza kuwa jukwaa la Kiswahili, chanzo cha machapisho na utafiti wa Kiswahili duniani.

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Dis-2020 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-2020 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 616 | 514 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 4 727 | 5 290 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 154 | 49 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22 | 24 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 261 | 268 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 8 300 | 4 000 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 19 205 | 15 766 |
| 12. Mali Nyingine | 5 064 | 4 867 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 918 | 1 037 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **39 267** | **31 815** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 18 683 | 15 802 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 941 | 836 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 417 | 294 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 425 | 281 |
| 27. Dhima Nyingine | 1 322 | 1 215 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **21 788** | **18 428** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **17 479** | **13 387** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30 912 | 30 912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (14 445) | (14 445) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3 988) | (3 080) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5 000 | - |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **17 479** | **13 387** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 389 | 296 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (266) | (266) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 45% | 42% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.0% | 1.8% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 101% | 98% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 48% | 49% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70% | 62% |
| - Ongezeko la Amana | 18% | 77% |
| - Ongezeko la Mali | 23% | 23% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 31-Dis-2020 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Dis-2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dis-2020 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dis-2019 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 807 | 721 | 2 765 | 2 936 |
| 2. Gharama za Riba | 334 | 98 | 694 | 547 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **473** | **623** | **2 071** | **2 389** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | (27) | (25) | (80) |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 192 | 144 | 388 | 454 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | 1 | 6 | 7 | 27 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 189 | 114 | 370 | 403 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 2 | 24 | 11 | 24 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1 571 | 1 578 | 6 472 | 7 735 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 708 | 708 | 2 801 | 3 337 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 863 | 870 | 3 671 | 4 398 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(906)** | **(784)** | **(3 988)** | **(4 812)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | 15 | - | 15 |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(906)** | **(799)** | **(3 988)** | **(4 827)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | | | | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(906)** | **(799)** | **(3 988)** | **(4 827)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 65 | 59 | 65 | 59 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -15 | -13 | -65 | -78 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-2%* | *-3%* | *-13%* | *-16%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-6%* | *-5%* | *-26%* | *-29%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *236%* | *206%* | *263%* | *289%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *2%* | *4%* | *8%* | *12%* |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Dis-2020 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dis-2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Dis-2019 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (906) | (1 153) | (3 988) | (4 812) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 389 | 379 | 1 413 | 1 710 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7 739) | (3 419) | (10 353) | 3 104 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2 881 | 6 876 | 7 610 | 3 284 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | (27) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 487 | 65 | 536 | (764) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (427) | 76 | 599 | (973) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | (270) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(5 315)** | **2 824** | **(4 183)** | **1 252** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (17) | - | (29) | (55) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | 1 121 |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(17)** | **-** | **(29)** | **1 066** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | - | |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo (Mtaji tangulizi) | 5 000 | - | 5 000 | 375 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **5 000** | **-** | **5 000** | **375** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | - | |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslir | (332) | 2 824 | 788 | 2 693 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5 781 | 2 957 | 1 557 | 1 585 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5 449 | 5 781 | 2 345 | 4 278 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2020 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Ziada nyingine | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30 912 | (14 445) | - | - | - | 16 467 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (3 988) | - | - | - | (3 988) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Mtaji tangulizi | 5 000 | - | - | - | - | 5 000 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 35 912 | (18 433) | - | - | - | 17 479 |
| **Mwaka Uliopita** | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30 912 | (9 976) | - | 179 | 179 | 21 294 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (4 827) | - | - | - | (4 827) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | 179 | - | (179) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | 179 | - | - | (179) | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 30 912 | (14 445) | - | - | - | 16 467 |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2020**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ........................ (Imesainiwa) | 22 Januari 2021 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ........................ (Imesainiwa) | 22 Januari 2021 |
| Patrick Mashallah (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ........................ (Imesainiwa) | 22 Januari 2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani | ........................ (Imesainiwa) | 22 Januari 2021 |
| 2/ Celestin Muganga | ........................ (Imesainiwa) | 22 Januari 2021 |

**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11**

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50 000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 7 500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1 300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 1 500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 100 000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6 000 |
| | (l) Stop payment | TZS 40 000 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 10 000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 10 000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10 000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| 2 | **Savings Accounts (Disclose for product specific types)** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5 000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 1 400 |
| | (c) Interim statement | TZS 1 500 |
| | (d) Account closure | TZS 20 000 |
| 3 | **Electronic Banking** | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| 5 | **Personal Loans** | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 0.77% p.a |
| | (i) Personal loans | 16% |
| | (ii) Overdrafts | 20% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

**Deposit Rates**

| | Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|---|
| | 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.0% | 2.5% |
| | 2 - 10Mln | 2.0% | 2.5% | 3.0% |
| | 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.0% | 3.5% |
| | 50 - 100 Mln | 3.0% | 3.5% | 4.0% |
| | 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.0% | 4.5% |
| | 300 - 500 Mln | 4.0% | 4.5% | 5.0% |
| | 500m - 1Bln | 4.5% | 5.0% | 5.5% |
| | Above 1 Bln | Contact Treasury | | |
| | **Savings Account - TZS** | **Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly** | | |
| | 0- 50k | 0.5% | | |
| | 50k - 1mln | 1.0% | | |
| | 1 - 10mln | 1.5% | | |
| | 10 - 100mln | 2.0% | | |
| | Over 1mln | 2.5% | | |

**Base Lending Rates**

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year) | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years) | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 years) | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard L. Makungwa | Chief Executive Officer | | 22 January 2021 |
| 2 | Leticia Ndongole | Ag. Head of Business Development & Marketing | | 22 January 2021 |
| 3 | Selemani Kijori | Head of Finance | | 22 January 2021 |

**Head Office**

**Mlimani Tower - Mezzanine Floor,
Sam Nujoma Road
P.O.Box 61002,
Dar es salaam
Phone: 022-2772954/7
email: info@mcb.co.tz
Customer Care No.:
0629331151|0629331755|0800750033**

**Mlimani Branch
Mlimani Tower - Ground Floor
Sam Nujoma Road
Dar es salaam**

**Samora Branch
Samora Avenue
Consolidated Holding Building Ground Floor**

**Regional Office - Morogoro
19, Plot E, Nkomo Street
Phone: +255 622 005 574
Morogoro**

**Regional Office - Mbeya
90, Plot L, Sokomatola Street
Phone: +255 766 903 575
Mbeya**

**Regional Office - Mwanza
18, Plot A, Kirumba Street
Phone: +55 788 138 238
Mwanza**

**Jipatie kadi yako ya Mwalimu Visa Sasa**



## HABARI KITAIFA


### TANGAZO LA ZABUNI UNUNUZI WA PAMOJA (BULK PROCUREMENT) WA VIUATILIF NA MAGUNIA KWA MSIMU WA 2021/2022
### ZABUNI NAMBA : 1 MAGUNIA/UNIONS/2021, 2. VIUATILIFU/UNIONS/2021

1. Vyama Vikuu vya Ushirika vinavyohudumia wakulima wa zao la Korosho vya **TANECU LTD, MAMCU LTD, TAMCU LTD, RUNALI LTD, CORECU LTD na LINDI MWAMBAO LTD** vinatangaza zabuni ya ununuzi wa pamoja wa Magunia na Viuatilifu kwa msimu wa 2021/2022.
2. Kwa idhini ya Bodi ya Vyama Vikuu hivyo, Mwenyekiti wa kamati ya zabuni ya ununuzi wa pamoja anatangaza zabuni shindani ya kitaifa (National Competitive Tendering- NCT) ya ununuzi wa Pamoja (Bulk Procurement) ya Magunia na Viuatilifu kwa ajili ya maandalizi ya msimu wa Korosho kwa mwaka **2021/2022** kama ifuatavyo: -

| LOTI | | MAHITAJI | UJAZO/UZITO | IDADI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | Magunia (Jute/Sisal – Kitani/Katani) | Idadi | 2,800,000 |
| 2 | i. | Salfa ya Unga yenye kiambata99 - 99.9% (g/Kg) | Tani | 29,473 |
| | ii. | Viuatilifu vya maji/kimiminika au chembechembe vya mguso/mfumo kwa ajili ya Ubwiriunga wa mikorosho. | Lita | 632,840 |
| | iii. | Viuatilifu vya maji/kimiminika au chembechembe vya mguso/mfumo Kwa ajil ya ugonjwa wa blaiti ya mikorosho. | Lita | 350,000 |
| | iv. | Viuatilifu vya maji/kimiminika au chembechembe vya mguso/mfumo kwa ajili ya udhibiti wadudu waharibifu wa mikorosho. | Lita | 412,862 |

3. Wanakaribishwa wazabuni wenye uwezo wa kusambaza magunia aina ya Kitani au Katani (Jute/Sisal). Wazabuni watakaosambaza magunia yaliyotengenezwa kwa katani (Sisal) watapewa kipaumbele zaidi.
4. Viuatilifu vyote vinapaswa kuwa vimetengenezwa hivi karibuni na lazima viwe angalau na miaka miwili ya maisha rufani.
5. Mzabuni mmoja anaruhusiwa kuomba LOT zote endapo atakuwa na vigezo stahiki kwa kila LOT.
6. Mchakato wa Zabuni hii utafanyika kwa njia shindani ya kitaifa (NCT) kwa mujibu wa Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya 2016 na ni zabuni ya wazi kwa Wazabuni wote wenye sifa zinazotakiwa.
7. Wazabuni wenye nia ya kushiriki, wanakaribishwa ofisi ya Katibu wa Kamati ya Ununuzi wa Pamoja iliyopo wilaya ya Mtwara Mtaa wa barabara ya TANU. Jengo la Ushirika wa Wakulima, Ofisi ya MAMCU Ltd ghorofa ya pili kwa ajili ya kuchukua Kitabu cha Zabuni (Tender Document) wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu kamili asubuhi (3:00) hadi saa kumi na nusu jioni (10:30) isipokuwa siku za Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za sikukuu.
8. Kitabu cha zabuni kitapatikana kwa kuandika barua kwa Katibu wa Kamati ya Ununuzi wa Pamoja ya kuomba kuuziwa kitabu cha Zabuni (Tender Document) kwa gharama ya shilingi za kitanzania 200,000/= ambazo hazitarudishwa (nonrefundable fees) na fedha zote zilipwe kupitia:-

**Jina: MAMCU Ltd**
**Akaunti Na: 01J1015468703**
**BENKI YA CRDB, TAWI LA MTWARA**

**Masharti ya Jumla kwa Mzabuni wa Viuatilifu ni kama ifuatavyo:-**

I. Mwombaji awe na Kampuni yenye uwezo wa kazi ya uuzaji na ugavi wa Viuatilifu vyenye ubora kwa ajili ya zao la Korosho. Ubora wa Viuatilifu uwe umethibitishwa na TROPICAL PESTICIDES RESEARCH INSTITUTE (TPRI). Cheti cha Uthibitisho wa Ubora wa Sampli za Viuatilifu (Certificate of Analysis) kutoka TPRI iwasilishwe kwa uhakiki.
II. Mwombaji awe tayari kupokea malipo yake baada ya biashara ya Korosho kufanyika;
III. Mwombaji atapaswa kuweka dhamana ya utekelezaji wa Mkataba (Performance Security in the form of Bank's Guarantee) kwa kiwango cha asilimia kumi (10%) ya bei ya Mkataba;
IV. Mwombaji awe tayari kusambaza Viuatilifu mapema kwa vyama Vikuu vya Ushirika kabla ya tarehe 30/04/2021;
V. Mwombaji aambatanishe Barua ya Mtengenezaji (Manufacturers Authorization Letter) ya Viuatilifu akiambatanisha na Cheti cha Ubora wa Viuatilifu kutoka nchi ya Mtengenezaji (Manufacturer).

**MASHARTI YA JUMLA**

I. Mwombaji aandike Barua ya Maombi akiainisha gharama ya Zabuni kwa kila kazi anayoomba na athibitishe kuwa atakuwa tayari kupokea malipo baada ya biashara ya Korosho kufanyika kwa mujibu wa mfumo wa stakabadhi ghalani.
II. Mwombaji awe na Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya usajili wa Makampuni.
III. Awe amelipa Kodi
IV. Aambatanishe Wasifu wa Kampuni yenye CVs za Wakurugenzi na vyeti vya Taaluma vya Watendaji wenye Uzoefu na Weledi wa kazi anayomba.
V. Picha tatu (3) ndogo (Passport size) za mmiliki wa kampuni.
VI. A Notarized and Registered power of Attorney
VII. Taarifa za Kibenki ikijumuisha pamoja taarifa ya ukaguzi kwa miaka mitatu mfulilizo **(2018, 2019 na 2020)**
VIII. Vivuli vya nyaraka muhimu (TIN, VAT, Tax Clearance na Stakabadhi ya malipo ya Kodi na Leseni ya Biashara).
IX. Mwombaji aambatanishe dhamana ya Benki (Credit line) ikionyesha uwezo wake wa kukopesheka kwa kiwango kisichopungua shilling Milioni 500 toka Benki yoyote hapa Tanzania.
X. Awe na wastani ya mauzo (Annual Turn Over) kwa miaka mitatu yasiopungua milioni 700
XI. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka miwili katika kufanya kazi zinazofanana kwa ukubwa na kwa thamani (size and Value) au walau sawa na asilimia 75% ya kazi hii inayotangazwa kwa mkataba mmoja (walau nakala mikataba miwili iambatanishwe kwa uhakiki wa kazi zilizofanyika)

9. Waombaji wawasilishe zabuni zao (nakala tatu, Nakala halisi na kopi mbili) zikiwa zimefungwa kwa umakini na kutiwa lakiri na kubainisha namba ya zabuni (1. Magunia/Unions/2021 au 2. Viuatilifu/Unions/2021). Zabuni zote zitafunguliwa mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, tukio ambalo litakuwa ni la wazi na wazabuni au wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria. Mwisho wa kupokea na kufungua zabuni ni siku ya **21 Tarehe 09/02/2021 saa 4:00 asubuhi** katika Ofisi ya MAMCU Ltd Mtwara Mjini.

Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-
Katibu wa Kamati ya Ununuzi wa Pamoja,
MAMCU Ltd,
S.L.P. 660, **Mtwara.**

Au yapelekwe kwenye ofisi ya Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika MAMCU Ltd iliyopo Mtwara mjini Jengo la Ushirika wa Wakulima, mtaa wa TANU Road.
**Meneja Mkuu,**
**MAMCU Ltd,**
**S. L. P 660, MTWARA**

10. Zabuni zote sharti ziambatanishwe na dhamana (Bid security in the form of Bank Guarantee) ya asilimia mbili (2%) ya thamani ya zabuni. Uhai wa dhamana ni siku thelathini (30) baada ya mwisho wa uhai wa Zabuni.
11. Zabuni zitakazochelewa kupokelewa hazitafikiriwa wakati wa tathmini bila kujali sababu zozote za kuchelewa.

..........................
**JAHIDA HASSAN SAID**
**MWENYEKITI WA KAMATI YA UNUNUZI WA PAMOJA VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA WA KOROSHO**


# Mbaroni madai ya ujambazi, yumo aliyetoroka kifungo cha miaka 30

**Na Boniface Gideon,** TANGA

WATU wanne wanaosadikiwa kuwa majambazi sugu waliokuwa wakitafutwa kwa muda mrefu, wamekamatwa mkoani hapa wilayani Korogwe, akiwamo anayedaiwa kuwa kiongozi wa genge la uhalifu ambaye alitoroka gerezani mwaka 2019 wakati akitumikia kifungo cha miaka 30.

Watu hao wamekamatwa mwishoni mwa wiki katika operesheni ya kikosi maalumu cha Jeshi la Polisi iliyofanyika usiku wa kuamkia Januari 25, katika eneo la Kibaoni, Mombo wilayani humo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, aliwataja watu hao kuwa ni Hamis Mbelwa (46), Haji Semkondo (42), Barnaba Simon (62) na Ally Babiwi, wote wakazi wa Wilaya ya Korogwe.

Akifafanua, Kamanda Chatanda alisema watu hao wamekuwa wakifanya uhalifu kwa kutumia silaha.

"Kwa mfano huyu jambazi Hamis Mbelwa, alikuwa ni mfungwa katika gereza kuu la mkoa wa Tanga Maweni na alihukumiwa miaka 30 jela mwaka 2015, katika hukumu iliyotokana na kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha huko Korogwe na alitoroka gerezani na kuungana na genge lake la uhalifu Juni 2019," alisema Chatanda.

Alisema baada ya kutoroka gerezani mwezi Agosti 2019, aliongoza kufanya uporaji wa kutumia silaha Hospitali ya Rosmin iliyopo wilayani Korogwe na kupora Sh. milioni nane.

Akizungumzia Barnaba Simon, maarufu Nyau spos, Chatanda alisema alikuwa mlinzi wa kampuni ya Gomba Estate, wilayani Korogwe na mshirika wa genge la uhalifu lililokuwa likiongozwa na Hamis Mbelwa na amekuwa akitumia silaha aina ya Shotgun yenye usajili namba 328932 ambayo hutumika kwenye matukio mbalimbali ya uhalifu.

"Huyu ni mlinzi, lakini ni mshirika wa genge la uhalifu la Hamis Mbelwa na amekuwa akiwakodishia silaha majambazi wenzake kwa Sh. 200,000 kwa siku kwa ajili ya utekelezwaji wa uhalifu," alisema Chatanda.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akikabidhi hati ya ardhi kwa wenza Ramadhani na Martha Zongo wakazi wa Bariadi mkoani Simiyu, kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanne kortini madai ya kughushi, rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

OFISA Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita na walimu watatu wa shule za msingi wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita wakishtakiwa kwa makosa manane ya kushawishi, kupokea rushwa na kughushi hati za mishahara.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa washtakiwa hao walighushi hati za mishahara ili waweze kujipatia mkopo kwenye benki ya Posta Sh. milioni 24.5 kitendo ambacho ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Washtakiwa hao ni Deogratius Kayanda (39), ambaye ni Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Paulo Matiasi (40), Mwalimu wa Shule ya Msingi Uhuru, Suzana Manyilizu (53), Mwalimu wa Shule ya Msingi Bugogo na Peter Chilangi (41), Mwalimu wa Shule ya Msingi Uhuru.

Washtakiwa wote kwa pamoja walifikishwa mbele ya hakimu wa mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza na waliposomewa mashtaka yao, walikana.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, alidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali.

Hakimu Kiiza alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Februari 9, mwaka huu kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali.

Hakimu alisema washtakiwa wawili, Deogratius Kayanda (39) ambaye ni Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Peter Chilangi (41), Mwalimu wa Shule ya Msingi Uhuru, walishindwa kutimiza masharti ya dhamana na wako mahabusu Gereza la Geita.

# Benki zatakiwa kwenda vijijini

**Na Said Hamdani,** LINDI

BENKI zinazohudumu mkoani Lindi, zimeshauriwa kuwa na utaratibu wa kutembelea wakulima vijijini kwa ajili ya kuwapa elimu ikiwamo ya ujasiriamali.

Lengo ni kuwafanya wawe na uelewa mkunwa utakaowasaidia kujitokeza kwa wingi kuhifadhi na kuomba mikopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Ushauri huo umelilewa na wakulima wanachama wa Chama cha Ushirika cha Msingi (KITUMIKI AMCOS) cha Manispaa ya Lindi, wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi.

Wakulima hao kutoka maeneo ya Kitumbikwera, Kineng'ene, Tulieni na Mitwero, walishauri hayo kufuatia wataalamu wa Benki za CRDB, NMB na NBC kuudhuria mkutano huo kuwapa elimu ya umuhimu wa kutumia taasisi hizo kuweka fedha na kuomba mikopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Said Rashidi, Selemani Daudi (Mkilwa) na Bakari Rashidi walisema kushindwa kwa wakulima walio wengi kuacha kutumia Benki kuhifadhi fedha zao zinazotokana na mauzo ya mazao yao, kunachangiwa zaidi na kutokuwa na elimu ya kutosha kufahamu umuhimu wake.

Walisema kama kila mmoja atakuwa na uwelewa wa kutosha, utunzaji wa fedha na upatikanaji mikopo inayotolewa na mabenki inapatikana kwa wakati, wakulima wengi watajitokeza na kuwa mstari wa mbele katika kutumia taasisi hizo za kifedha, ikiwemo kuomba mikopo kuendeleza kilimo chao.

Aidha, wajumbe wa Mkutano Mkuu wa KITUMIKI AMCOs wamewashauri wataalamu wa benki zinazohudumu mkoani Lindi kutoendelea kubaki ofisini, badala yake wajitoe kufuata wateja (wakulima) wanaowahitaji kwenye maeneo yao na kuwapa elimu ya ufahamu.

Rashidi alisema wakulima wanasita kujitokeza kuomba mikopo wakihofia kupoteza mali zao walizozitafuta kwa shida pale watakaposhindwa kurejesha mikopo waliyochukua kwa wakati unaohitajika.

Mkilwa aliwashauri watendaji wa benki kuharakisha utoaji wa mikopo kwa wakulima wanaojitokeza kuomba ili waweze kuwahi shughuli zao za kilimo badala ya kusubiri kwa muda mrefu.

Wakijibu hoja za wanachama hao, watendaji wa benki hizo, Samuel Sunza (CRDB), Ndaki Madata (NMB) na Jovin Mapunda (NBC) walikiri kuwapo kwa upungufu huo, huku wakiahidi kuyafanyia kazi.

# Marufuku michango ya ovyo shuleni yasisitizwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amepiga marufuku michango aliyoiita ya ovyo ovyo kwa wanafunzi shuleni kwa kuwa serikali haitaki kuwakwaza wananchi.

Majaliwa alisema michango ambayo wanafunzi hugizwa na walimu wanapojisikia ni marufuku, ila michango itakayoruhusiwa ni iliyopitishwa na kamati za shule na kupewa baraka na wakuu wa wilaya.

Akizungumza jana na wananchi wa Ifunda Wilaya ya Iringa katika mkutano wake wa hadhara, alisema lengo la serikali kupiga marufuku michango hiyo holela ni kutaka kila mtoto apata elimu.

Alisema serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya elimu, na mwezi uliopita iliajiri walimu 8,000 na sasa imetangaza ajira 3,000.

Alisema serikali imefanya hivyo na itaendelea kuweka mazingira mazuri ya elimu.

Aidha, Majaliwa alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Iringa kushughulikia tatizo la uhaba wa maji katika Shule ya Sekondari Lyandembela kutokana na kuendelea kukosa maji.



Kaimu Ofisa Vijana Mkoa wa Singida, Frederick Ndahani (wa pili kushoto), akizungumza na walimu wa ufundi wa Shule ya Msingi Makiungua iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, alipoitembelea juzi, kwa lengo la kukagua uwezeshwaji mafunzo na ujuzi kwa vijana. **PICHA: DOTTO MWAIBALE** . **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# TMDA yajigamba urahisi uagizaji dawa, vifaa tiba

**Na Devota Mwachang'a**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Kanda ya Ziwa imefanikiwa kuharakisha kasi ya uingizaji na utoaji wa mizigo ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya forodha vya mipakani kupitia ukaguzi unaofanyika kabla ya kuziruhusu kuingia au kutoka nchini.

Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa, Sophia Mziray, aliyasema hayo hivi karibuni wakati akizungumza na waandishi wa habari jinsi mamlaka inatimiza majukumu yake kiudhibiti na ukaguzi wa maeneo yanayozalisha, yanayouza, yanayohifadhi na kutoa huduma ya dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba.

Alisema katika ukaguzi wa mipakani mzigo utakaokuwa umekidhi vigezo vyote utaruhusiwa, lakini usiokidhi utazuiliwa kupewa kibali cha kurudishwa kwenye nchi ulipotoka ama kuteketezwa.

"Mkaguzi aliyepo mpakani anakagua bidhaa na nyaraka zote zilizoambatana nao ikiwamo kibali kilichotolewa na mamlaka kupitia mfumo wa kielekroniki. Mfumo huu umetusaidia kudhibiti kwa kiasi kikubwa matumizi ya vibali vya kughushi kwa wafanyabiashara wasio waaminifu," alisema.

Aidha, Mziray aliwashauri wananchi kutoa taarifa za wafanyabiashara wasio waaminifu ili kuokoa maisha ya watumiaji wa bidhaa za dawa kwa kuziondoa sokoni dawa zisizo salama na kusalia na zile zeye ubora, salama na zenye ufanisi.

"Napenda kuwaasa wafanyabiashara wasiowaaminifu kuacha kufanya biashara haramu ya dawa, vifaa tiba au vitendanishi. Watambue kwamba TMDA iko macho na inaendelea kuweka nguvu kubwa ya kuwabaini nakuwachukulia hatua stahiki za kisheria," alitahadharisha.

Wakati huo huo, Mkaguzi wa Dawa kutoka TMDA Kanda ya Ziwa, Mtani Njegera, alisema mamlaka hufanya uteketezaji wa dawa na vifaa tiba visivyo salama, uteketezaji huo ni kwa hiari ya wafanyabiashara au bila hiari kwa amri ya mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba na mwongozo wa uteketezaji wa dawa wa Mwaka 2009.

"Uteketezaji wa dawa hufanyika kwa kuzingatia sheria zilizopo ambazo hulenga kulinda usalama mazingira na viumbe vilivyomo. Pamoja na mwongozo wa uteketezaji salama wa dawa nchini, mamlaka pia huzingatia Sheria ya Baraza la Mazingira nchini (NEMC)," alibainisha.

Njegera alisema mamlaka huwajibika kuzitaarifu taasisi au mamlaka zingine zinazohusika ili kushiriki katika uteketezaji. Baadhi ya taasisi ni Jeshi la Polisi, Mfamasia, Afisa mazingira, Usalama wa Taifa, na mwakilishi wa mmiliki wa dawa au vifaa tiba vinavyoteketezwa.

# DC aagiza kasi ya ujenzi wa madarasa kidato cha 1 Moro

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZAZI na walezi wa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Morogoro wametakiwa kuongeza kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kusaidia wanafunzi wanaosomea kwenye vyumba vya maabara kwa sasa kurejea madarasani ifikapo Februali 28, mwaka huu.

Wanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule za sekondari wilayani humo wameshaanza masomo baada ya kukamilika kwa baadhi ya vyumba vya madarasa, huku vyumba vya maabara pia vikitumika kusaidia wanafunzi hao.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, alisema hayo jana baada ya kupokea msaada wa madawati 50 yenye thamani ya shilingi milioni 5 yaliyotolewa na benki ya NMB kanda ya Mashariki kwa Shule ya Sekondari Kingolwira iliyopo wilayani hapa.

Msulwa alisema kukamilika kwa baadhi ya vyumba vya madarasa katika shule za Sekondari kumeonyesha nia njema ya wananchi kujitolea sambamba na kasi ya ujenzi inayoendelea ambapo matumizi ya vyumba vya maabara yatakwisha mwishoni mwa Februali mwaka huu vyumba vya madarasa vinavyohitajika vitakapokamilika.

Alisema aliishukuru NMB kwa msaada huo ambapo alisema ipo misaada inayotolewa lakini inayogusa huwa ni ya maana sana, na kwamba msaada huo umetolewa wakati mwafaka.

Aidha, alisema wastani wa sasa wa wanafunzi kwa darasa moja ni 50 na kwamba madawati hayo 50 yaliyotolewa yanatosha kabisa kwa darasa zima.

Msulwa alisema fedha wanazotoa NMB zipo katika mipango yao ambapo wanaouwezo wa kubadilisha mipango na kupeleka wanakotaka, lakini wameamua kuwekeza kwenye elimu jambo ambalo linapaswa kuungwa mkono na jamii kupitia kufungua na kuweka fedha kwenye akaunti za NMB ili kuwezesha kukua kwa makusanyo hayo.

Aliwataka walimu na wanafunzi kuhakikisha wanalinda walichopewa ili kuepuka kuharibu misaada inayotolewa mapema na kuondoa dhana ya misaada husika.

"Wapo wanafunzi badala ya kukaa kwenye kiti anasimama kwenye kiti na wengine badala ya kukaa kwenye kitu anatembea kwenye kiti, wekeni utaratibu wa kuwachkulia hatua pindi mtapowakamata wanaleta uharibifu," alisema.

Naye Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Anneth Kwayo, alisema NMB kwa miaka 8 mfululizo sasa imeamua kutenga asilimia 1 ya mapato yake ya kila mwaka kusaidia jamii katika nyanja za afya, elimu na majanga.

Alisema kwa mwaka 2020 ilitumia kiasi cha Sh. bilioni 1 katika kusaidia jamii kupitia nyanja au sekta hizo katika mikoa iliyopo kwenye kanda ya mashariki.

Kwayo alisema katika kuunga mkono suala la elimu bure lililoibuliwa na Rais John Magufuli wameona ni vema kuwekeza kwenye elimu kwani hata baadaye wanaweza kupatikana viongozi mbalimbali wa nchi.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Kingolwira, Shangwe Mgheni, aliishukuru NMB kwa kuwapatia msaada huo ambapo alisema umeweza kuwasaidia kukabiliana na upungufu wa madawati waliokuwa nao.



Mhandisi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Elibariki Mwendo, akitoa maelezo namna wanavyotekeleza mradi wa miundombinu ya skimu ya umwagiliaji kwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge (katikati), pamoja na Kaimu Mkuu wa Utawala wa Jeshi hilo, Kanali Hassan Mabena walipotembelea kambi ya JKT Chita mkoani Morogoro. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wachanjwa kidole tumbo, bawasili

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAGONJWA 35 wamefanyiwa upasuaji katika Hospitali ya Chakechake Pemba baada ya kusumbuliwa na ugonjwa wa bawasili na kidole tumbo (appendex) kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka 2020.

Kati ya wagonjwa hao waliofanyiwa upasuaji wanawake ni 20 na wanaume ni 15.

Akizungumza na Nipashe, daktari bingwa wa upasuaji katika hospitali hiyo, Yunus Pandu Buyu, alisema, mwaka 2019 walifanyiwa upasuaji wagonjwa 19 na mwaka 2020 walifanyiwa wagonjwa 16.

"Kati ya wagonjwa hawa 35, waliofanyiwa upasuaji kwa ugonjwa wa bawasili ni watu 13 na wagonjwa 22 walifanyiwa kwa ugonjwa wa kidole tumbo, ambapo wanawake waliofanyiwa upasuaji wa bawasili ni nane na kidole tumbo ni 12, wakati wanaume waliofanyiwa upasuaji wa bawasili ni watano na kidole tumbo ni kumi," alifafanua daktari huyo.

Alisema kwa kipindi hicho cha miaka miwili, jumla ya wagonjwa 153 walifika hospitalini hapo kwa ajili ya uchunguzi, ambapo 35 tu ndio waliofanyiwa upasuaji, na kwamba hakuna vifo vilivyotokea.

"Waliofika kutaka huduma ambao wanasumbuliwa na ugonjwa wa bawasili walikuwa 103 na kidole tumbo ni 50, ambapo wagonjwa 118 kati yao walipatiwa dawa na kurudi nyumbani," alisema.

Dk. Yunus alieleza kuwa bawasili inasababishwa na watu kula vyakula ambavyo havijakobolewa, hivyo ipo haja ya kula vyakula hivyo na laini ili kuepukana na ugonjwa huo."

Kwa upande wa kidole tumbo, daktari huyo alisema husababishwa na maambukizi ya bakteria ambapo kidole hicho huvimba na kupelekea tumbo kuuma chini upande wa kulia, kichefu chefu, kutapika na homa kali, dalili.

Akizungumzia changamoto zinazowakabili katika ufanyaji wa kazi zao ni wagonjwa kupoteza kumbukumbu, kufika hospitali katika hali ya dharura na kutokuwa na chumba maalumu cha upasuaji, hali ambayo wakati mwingine analazimika wagonjwa kuwasafirisha.

## Wazazi wahimizwa kusomesha watoto

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wamehimizwa kuwasomesha watoto wao kwa hali na mali kwa kuwa elimu ndiyo urithi pekee utakaokuwa na msaada kwa mtoto kwenye maisha yake yote.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki kwenye Kanisa la Mlima wa Moto na mmoja wa wakurugenzi wa Shule za St. Mary's, Muta Rwakatare, wakati wa ibada ya shukrani kwa shule hizo kufanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa.

Muta alisema uwekezaji mkubwa uliofanywa na mwanzilishi wa shule hizo, Hayati Mchungaji Dk. Getrude Rwakatare umekuwa ukombozi kwa Watanzania wengi nani alama ambayo haitafutika.

Alisema mama yake aliamua kuanzisha shule za mchepuo wa Kiingereza baada ya kuona idadi kubwa ya wanafunzi kutoka Tanzania kwenda Uganda na Kenya kwa ajili ya kutafuta elimu hivyo kutumia gharama kubwa na muda.

"Siku moja mama alikuwa akisafiri kwenda Kenya kwenye shughuli zake njiani aliwaona watoto wengi wakisafiri wengine wakiwa wadogo kiasi cha kuhitaji uangalizi wa karibu wa wazazi, ilimuuma sana na tangu wakati huo ndipo alipoamua kuanzisha shule ili wasomee hapahapa," alisema Muta.

Mkurugenzi mwingine wa shule hizo, Dk. Rose Rwakatare, alisema wameamua kutoa sadaka ya shukrani baada ya shule hizo kufanya vizuri kuanzia darasa la nne, la saba, kidato cha pili na kidato cha nne na kwamba licha ya ugonjwa wa corona mwaka jana hawakutetereka.

"Mwaka jana tulimpoteza mwanzilishi wa shule hizi, Mchungaji Getrude Rwakatare, lakini kwa sababu alituwekea misingi mizuri ya kiongozi hatukutetereka tulisimama imara na shule ziko vizuri na zinaendelea kuwa na matokeo mazuri," alisema Rose ambaye ni mtoto wa kwanza wa Hayati Mchungaji Getrude Rwakatare.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 26, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

Waundwa mkakati kuwawezesha wafanyakazi, waajiri kujitambua



Ukurasa 13

## MARTHA MGANGA: 'Aliyeonja mauti' na sasa anawaokoa wenye ualbino

ELIMU

NA GWAMAKA ALIPIPI

# JANGA DAWA ZA KULEVYA

- Chanzo maradhi yasiyoambukiza, ugaidi
- Kitisho uchumi, diplomasia, mazingira

DAWA za kulevya zinaendelea kuwaharibia maisha ya watumiaji kila kukicha na ndicho chanzo cha maambukizi ya maradhi yasiyoambukiza kama moyo, akili na figo wakati yanayoambukizwa ni kama Kifua Kikuu (TB) na homa ya ini.

Wanaojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya wanakuwa hawajui, lakini linapokuja suala la kujiondoa kwenye uraibu, uhakika wa kufanya hivyo haupo. Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, inatoa elimu kwa vijana jinsi ya kujikinga na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kueleza madhara ya matumizi yake.

Kamishna Msaidizi wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Dk. Cassian Nyandindi, anabainisha hayo katika mahojiano na Nipashe yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam. Anasema madhara ya matumizi ya dawa za kulevya ni makubwa yanayoweza kuainishwa katika makundi mbalimbali.



Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), James Kaji, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu dawa za kulevya. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

### ATHARI KIAFYA

Anasema athari zake ni lukuki zikiwamo mtumiaji anazozipata papo kwa hapo na nyingine za muda mrefu.

Mtaalamu huyo anaeleza kwamba watumiaji wa dawa za kulevya wanachangia kueneza Virusi Vya Ukimwi (UKIMWI). Ni kutokana na kupokezana vifaa vya kujidunga mfano sindano, anayetumia dawa akili yake inakuwa haipo sawa sawa, hivyo hata umakini wa kufanya mapenzi unakuwa mdogo bila kutumia kinga. Kwa kufanya, ngono zembe husababisha kusambaa virusi vya homa ya ini aina ya 'hepatitis' B na C inayoambukizwa kama UKIMWI kwa njia ya kujamiiana, kugusa majimaji za mwili na kujichoma sindano kama hizo.

Anaeleza kuwa watumiaji wa dawa za kulevya wanaathirika na magonjwa ya mapafu kama vile Kifua Kikuu (TB) kutokana na wengi kujificha sehemu zenye hewa kidogo, hivyo moshi wanaovuta unawaletea madhara ya magonjwa kama TB, lakini wakati mwingine watumiaji hao wanabadilishana sigara na kuambukiza maradhi yanayoshambulia kinywa na mapafu.

Dk. Nyandindi anasema: "Takwimu za mwaka jana zinaonyesha kuwa kila Watanzania 1,000 mmoja au wawili wana TB , lakini takwimu zetu katika kliniki za waathirika za dawa za kulevya zinaonyesha kuwa kwenye kila watu 1,000 wanaojidunga 65 hadi 110 wana TB."

Anaeleza kuwa magonjwa ya akili yapo kwa kiasi kikubwa kwa waathirika wa dawa za kulevya na takwimu zinaonyesha kuwa wanaokuja kutibiwa kutokana na matumizi hayo karibu asilimia 30 hadi 35 wanakuwa na tatizo la akili.

"Mfano mtu anayetumia bangi mwanzoni anakuwa na akili nzuri, lakini baada ya matumizi ya muda mrefu anaanza kuwa kichaa. Dk. Nyandindi anasema na kuongeza kuwa watumiaji wa dawa za kulevya wanakumbwa na maradhi ya ngozi kwa sababu hawaogi wala kubadilisha mavazi.

Anabainisha kuwa magonjwa ya kinywa yanawakumba pia hususani ni wa mirungi kutokana na namna wanavyoijaza midomoni, wengi hawapigi mswaki na kwamba idadi kubwa wanakumbwa na vifo vya ghafla kutokana na namna wanavyochanganya dawa hizo.

### MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA

"Magonjwa yasiyoambukiza ya ini, figo na moyo yameongezeka mno, idadi kubwa ni watumiaji wa dawa za kulevya kwa sababu dawa wanazozitumia zinakwenda kufanya kazi kwenye ini, figo na moyo. Uchakataji wake unategemea ini, figo ..." anasema Dk. Nyandindi na kuongeza:

"Mfano mtu akitumia cocaine, inachakatwa kwenye ini, utoaji wa uchafu unafanyika kwenye figo, madhara yake yanasukumwa na damu kazi inayofanyika kwenye moyo. Hata bangi hutolewa kwa njia ya mkojo na yote hufanyika kwenye figo," anaeleza Dk. Nyandindi.

### ATHARI KIUCHUMI/KIJAMII

Kamishna Msaidizi wa Kinga na Tiba, anaeleza kuwa watumiaji wa dawa za kulevya wanaleta athari kiuchumi, kwa mfano, mtu wa kawaida anataka kununua nyumba kwa kiasi fulani cha fedha ambacho wameshakubaliana na muuzaji, lakini anatokea mfanyabiashara dawa za kulevya kwa vile ana fedha nyingi anatoa kiasi kikubwa na kumzidi mnunuzi wa kwanza na kusababisha umaskini na hali duni kwa watu wenye kipato halali japo kidogo.

Akizungumzia athari kwenye jamii anasema familia nyingi zinasambaratika, kwa sababu mama asiyetumia dawa za kulevya hawezi kuishi na mwenza anayetumia mihadarati, hivyo ugomvi kati yao hauishi. Baba anampiga mama matokeo yake yanaweza kuwa vifo, kuachana, watoto wanasambaratika, yatima na wategemezi wanaongezeka.

Anasema endapo mama anayetumia dawa za kulevya akipata ujauzito, akijifungua watoto wanakuwa na upungufu, lakini maadili katika jamii yanapungua kutokana na matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vya uhalifu kama wizi, uporaji, ujambazi na utoro shuleni vinaongezeka.

### KIDIPLOMASIA/MAZINGIRA

Akizungumzia taswira ya nchi kimataifa Dk. Nyandindi anasema idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya ikiwa kubwa inachafua sura ya nchi kimataifa na kwamba raia wa nchi hiyo wanaposafiri kwenda taifa fulani, wakifika uwanja wa ndege wanadhaniwa wamebeba dawa za kulevya, wanapekuliwa sana kuliko abiria wengine, anasema Dk. Nyandindi.

Na kwa upande wa mazingira anasema matumizi ya dawa za kulevya yanaleta athari kimazingira, akitolea mfano wa namna bangi inavyolimwa sehemu zilizojificha zinasababisha kuharibu mazingira, vyanzo vya maji na uoto wa asili na kwamba wakulima wa mimea inayozalisha dawa za kulevya wanateketeza misitu, wanyama wanakimbia

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Serikali inavyolea, kuibua wanasayansi wa ndani

SAYANSI, teknolojia na ubunifu vinatajwa kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya elimu, ya kiuchumi na kijamii na kutokana na umuhimu wake, serikali hushindanisha wabunifu kwa lengo la kupata wabunifu na kazi zinazoweza kuendelezwa kwa tija kukuza utaalamu.

Mashindano hayo hufanyika kila mwaka yakihusisha makundi ya wabunifu na wadau wa sayansi na teknolojia katika nyanja mbalimbali nchini, ili kuhamasisha na kuleta mwamko wa kuibua na kuendeleza teknolojia na ubunifu miongoni mwa Watanzania.

Baadhi ya yale ambayo wabunifu wamewahi kushindanishwa, ni kutengeneza vitu na kutoa mawazo yanayolenga kutatua matatizo mbalimbali katika sekta za afya, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na elimu, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Maulilio Kipanyula.

Anaongeza kuwa hadi kufikia mwaka juzi, serikali imetumia Sh. bilioni 50.55, kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu na kufadhili watafiti na wahadhiri katika mafunzo ya shahada ya uzamili na uzamivu.

Anasema hayo katika warsha ya siku moja kwa waandishi wa habari, inayofanyika jijini Dar es Salaam na kuongeza kwamba, serikali inawatambua wabunifu kuanzia ngazi ya chini ili kazi zao zinufaishe taifa na wao wenyewe wajikwamue kiuchumi.

Aidha, anawahimiza Watanzania kubuni na kugundua teknolojia ambazo zitasaidia nchi kupiga hatua kimaendeleo, ili kufikia uchumi wa viwanda na pia kuhamasisha watafiti wasiishie kusambaza matokeo ya utafiti bali pia wauweke kwa namna ambayo utawafikia walengwa kwa lugha rahisi.




Helikopta iliyobuniwa na Adam Kinyekire wa Tunduma mkoani Songwe. **PICHA: MTANDAO**

Miongoni mwa wabunifu walionufaika na Sh. bilioni 50 ni Adam Kinyekire, aliyepata Sh. milioni 99 kwa ajili ya kuendeleza utafiti wa kutengeneza helikopta, uwekezaji unaohusisha kuimarisha karakana.

Aidha, fedha hizo zimelenga kuongeza ubunifu, utafiti na kuibua teknolojia zaidi na pia ili kumsaidia serikali imemuunganisha na Shirika la Nyumbu la Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) la Automotive Technology Centre (TATC), lililoko Kibaha kama njia ya kuendeleza ubunifu wake, anasema Profesa Kipanyula.

Mtaalamu wa Fizikia Edwin Konzo, anasema wabunifu wengi zaidi wanatakiwa kujitokeza kila mashindano yanapofanyika ili kazi zao ziweze kutambuliwa na kuendelezwa kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla na kwamba teknolojia na ubunifu ndilo eneo muhimu zama hizi za sayansi na teknolojia.

Anasema kupitia mashindano, serikali inaibua kutambua na kuendeleza ubunifu na ugunduzi unaofanywa na Watanzania hususani wale wa ngazi za chini na inatoa nafasi kwa wahusika hao kujitangaza na kujulikana na wadau wa ubunifu wa ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Mawasiliano serikalini, Sylivia Lupembe, anasema, kushindanisha ubunifu ni mkakati wa serikali ambao unalenga kuwaibua na kuwafikia watu wengi zaidi wanaoshiriki katika mashindano kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya ufundi stadi, vyuo vya ufundi wa kati, vyuo vikuu, taasisi za utafiti na maendeleo na mfumo usio rasmi. “Mashindano haya ni chachu ya ubunifu wa teknolojia, hivyo Watanzania zaidi wanatakiwa kutumia teknolojia, kwa kuwa ni kichocheo cha maendeleo ya haraka katika sekta ya huduma.” Anasema Sylvia.

Anaongeza kuwa kupitia mashindano ya ubunifu, washindi wanapata kipato kutokana na kiwango cha fedha ambacho kinatolewa na kwamba serikali itazidi kuendeleza ubunifu ili uwe bidhaa na uchangie katika kukuza uchumi na maendeleo ya taifa.

Anasema, kwa utaratibu huo, ana uhakika wabunifu wengi zaidi wanaweza kuwa wanajitokeza kila mashindano yanapofanyika, kwa kuwa mbali na kuongeza ubunifu wananuifaka kwa kazi zao.

Suala la ubunifu, ni miongoni mwa mambo yanayopewa kipaumbele katika ilani ya CCM ni pamoja na kukuza sayansi, teknoloja na ubunifu ili vitumike kikamilifu kuendesha sekta za kukuza uchumi na kuleta maendeleo.

Katika ilani hiyo serikali imeahidi kuimarisha mfumo wa uratibu wa shughuli za sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia kwenye ujenzi wa uchumi imara na endelevu na kutenga fedha ili kusomesha Watanzania nje na ndani ya nchi katika vyuo bora duniani kwenye sayansi, teknolojia na tiba ili kupata maarifa bora na ujuzi utakaochochea maendeleo nchini.

Ilani inasema kuwa serikali itaweka mazingira wezeshi kwa wataalamu wabobezi kutoka nje kuja kufanya kazi nchini, ili kuhawilisha (kuhamisha) maarifa na teknolojia kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Ahadi nyingine ni kuweka kipaumbele katika kujenga na kuendeleza uwezo wa Watanzania na kuimarisha matumizi salama ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika maeneo ya kimkakati, ikiwamo matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia na maendeleo ya teknolojia ya kidijitali.

Maelekezo mengine ya CCM kwa serikali, ni kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kusimamia na kuendeleza masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kuratibu uwekezaji utafiti unaochochea ugunduzi na utakaowezesha nchi kupunguza utegemezi wa teknolojia zinazotoka nje.

---

# JANGA DAWA ZA KULEVYA

**INATOKA UK.11**

na kusababisha ukame na mmomonyoko wa ardhi.

“Watumiaji wa dawa za kulevya kwa kujidunga wanatupa ovyo sindano na mabomba na vifaa vingine vya kuandaa dawa hizo zikiwamo chupa.”

**UHALIFU, UKOSEFU USALAMA**

Anapozungumzia masuala ya uhalifu, Dk. Nyandindi anasema vijana wengi wanaojiingiza katika vikundi vya kigaidi vya kitaifa na kimataifa wengi wao ni watumiaji wa dawa za kulevya na kwamba hakuna mtu mwenye akili timamu anayejiingiza katika vikundi hivyo bila kutumia vichocheo kama dawa hivyo.

Dk. Nyandindi anasema: “Kuna utafiti umewahi kufanyika unaoeleza kwamba vijana wa kikundi cha kigaidi cha Bokoharamu cha Nigeria asilimia 65 wanatumia dawa za kulevya”.

**UDHIBITI MAJUKUMU YA MAMLAKA**

Dokta Nyandindi anasema Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ina majukumu makuu manne yakiwamo kuzuia uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Aidha kuhakikisha jamii haiingia katika matumizi ya dawa za kulevya kwa kupata elimu sahihi.

Anasema jukumu jingine ni kupambana na kutokomeza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya, kuimarisha ushirikiano katika mapambano kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda pamoja na kimataifa na kwa kushirikiana na wadau wengine hutoa elimu juu ya madhara ya dawa hizo katika makundi mbalimbali ya kijamii ili isijihusishe na matumizi ya dawa hizo.

Anasema elimu hiyo hutolewa kupitia vyombo vya habari, machapisho, maadhimisho ya kitaifa, semina na makongamano: “Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2019, mamlaka ilitoa elimu kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani kitaifa. Katika maadhimisho hayo elimu ilitolewa katika maeneo yaliyokithiri kwa matumizi na biashara ya dawa za kulevya katika Jiji la Tanga, ambako vijana takribani 180 waliopo katika mazingira hatarishi ya kujihusisha na dawa za kulevya walipata elimu na kwa wale waliopata uraibu wa dawa hizo walihamasishwa kujiunga na tiba.”

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# MARTHA MGANGA: 'Aliyeonja mauti' na sasa anawaokoa wenye ualbino

BAADA ya kuzaliwa na ualbino na kuonekana kama mtu asiyekubalika ndani ya jamii Sista Martha Mganga, anaweka nadhiri ya kuwasaidia watu wanaozaliwa na hali ya ualbino, akifuatilia maisha yao kuanzia wanapozaliwa, kuwapa faraja walioteswa, kuwasaidia kupata elimu, huduma za afya na kulinda ustawi wao.

Anapozungumza na Nipashe hivi karibuni, Sista Martha Mganga, aliyeanzisha Taasisi ya Peace Maker for Albinism and Community, anafanya shughuli zake mkoani Arusha, anasema anawalea na kuwasaidia wenye ualbino baada ya kuweka ahadi kwa Mungu, anayesema alimnusuru na mauti na mateso mengi, akiamini alifanya hivyo ili amtumie kuwasaidia watakaozaliwa na hali hiyo.

Akikumbusha baadhi ya changamoto alizopita, anasema alizaliwa mapema miaka ya 1960 mkoani Arusha na wazazi wakata mkonge. Baba na mama walikuwa na rangi nyeusi, lakini walipata watoto watatu wenye ualbino na huo ukawa mwanzo wa maisha magumu ya huzuni na uchungu kwake na ndugu zake pamoja na wazazi, lakini mama aliyenyanyasika na kuteseka zaidi.

Anasema; "Mama ndiye aliyeelemewa na mzigo akihukumiwa kuwa na hatia kwa sababu yeye na mumewe hawana ualbino inakuwaje amepata watoto wanaoishi na ualbino? Anahukumiwa kuwa pengine siyo mwaminifu kwenye ndoa yake, anabebeshwa lawama na familia, ndugu na jamii inayomzunguka."

Martha anasema alipokuwa na kujitambua alifahamu fika kuwa hakubaliki kwenye familia. Akienda shuleni wanafunzi wanamwogopa, mitaani inazingirwa na watu wenye imani potofu wanaosema kuwa yeye si binadamu wa kawaida ni mtu anayepotea kimaajabu.

Darasani anakutana na walimu wanaomfuka asikae mbele kwa fikra potofu, wasiotaka mwenye ualbino awakaribie. Hivyo, anasema licha ya kuwa na uoni hafifu anafukuzwa akae nyuma, anaadhibiwa, kufokewa na kudhalilishwa akiitwa mjinga.

"Yote hayo niliyaweka moyoni. Nikaangalia adha na manyanyaso anayopata mama yangu kwa ajili yetu. Anafukuzwa na baba, lakini bado anaendelea kutubeba na kututunza niliona hakuna sababu ya kuendelea kuishi. Nilipanga kumaliza maisha yangu na kuwaacha kwa amani hasa mama anayebeba lawama zote." Anasema mwanaharakati huyo.

Mwanaharakati huyo alizaliwa na wazazi kutoka Dodoma waliohamia katika Kijiji cha Doli karibu na Usa Riva mkoani Arusha, lakini akakulia Kijiji cha Makiba kwenye kilimo cha mkonge ambako wazazi wake walikuwa wakifanyakazi kwenye mashamba ya zao hilo anasimulia jaribio la kujiua.



Mama Martha (kushoto) na baadhi ya watoto anaowalea nyumbani kwake Njiro, wakianza safari ya kuelekea shuleni mapema mwezi huu, wakiwa na mafuta ya kuwakinga na mionzi ya jua, madaftari na vifaa vya shule tayari kwa masomo. **PICHA: PEACE MAKER FOR ALBINISM**

### KUJIMALIZA

Anasema akiwa na miaka 21, alikata tamaa baada ya kuona maisha hayana maana. Aliamua kujimaliza kwa kujitupa mtoni usiku wa manane, wakati wa mafuriko ili apotee iwe kuliwa na mamba, kufukiwa mchangani au lolote ili kuachana na maudhi na maisha yaliyojaa kukejeliwa, kuchukiwa na kunyanyapaliwa.

"Nilitoroka nyumbani kijijini kwetu Makiba saa 12 jioni nilitembea usiku wote nikijua kuwa kama nitaondoka mchana wataniona na kunirudisha. Nilijitosa usiku nikaelekea ulipo Mto Nduruma. Niliufikia baada ya kutembea muda mrefu porini nikiwa mwenyewe. Usiku wa manane nilifika mtoni. Nilisikia sauti ya maji ikivuma kwa nguvu ulikuwa umejaa na kufurika nilijitupa mtoni ili uwe mwisho wangu. Lakini haikuwezekana Mungu aliniokoa. Maji yalinipokea na kunirusha juu ardhi upande wa pili sehemu kavu nikiwa salama. Nilisikia sauti ikiniambia usiogope bado ninakupenda. Nilikuwa salama na asubuhi watu walinikuta na kuniondoa. Huo ukawa mwanzo mpya wa maisha yangu." Anasema Martha.

Aliingia mtoni kwa kukata tamaa kwa sababu hakukubalika popote kijijini, shuleni anakimbiwa na kuogopwa, lakini anapigwa na walimu na mama yake anateseka kwa vile hawezi kumuacha.

### PAMBAZUKO JIPYA

Baada ya kunusurika aliahidi kuwasaidia wenye ualbino na kuanzia mwaka 1986 akiwa na miaka 23 alianza kazi ya kuwasaidia watoto na jamii ya wenye ualbino: "Nilimwambia Mungu umenikoa, umenilinda, kama utanitunza nisife katika umri mdogo, ukanipa nguvu na uwezo nitawatunza wanaoishi na ualbino. Nitawafariji, nitawahudumia na kuwasaidia kuvuka kwenye changamoto wanazopitia ambazo najua haziwezi kukosekana."

Anasema akiwa Arusha alianzisha huduma ya kuwasaidia wenye ualbino, wakiwamo wagonjwa, kuwatafuta na kuishi nao kwenye chumba chake, kuwalisha chakula, kuwatibu, kuwasaka na kuwahifadhi watoto waliotelekezwa na kuwasaidia kupata shule za kusoma iwe bweni au popote juhudi zilifanywa kwa kuomba uhisani si kwa kulipia.

"Niliwatia moyo, nikawasaidia kuelewa kuwa wapo kwa kusudi la Mungu, si kwa mapenzi mtu wala jamii," anasema na kuongeza kuwa alikuwa hana kipato, lakini alikuwa mtumishi wa Kanisa la Anglikani akifanyakazi kanisani.

Kuanzia mwaka 2015 amekuwa akiwahudumia wenye ualbino takribani 160 zaidi ni wanafunzi wanaotoka mikoa mbalimbali wanaopatiwa matibabu, kusomeshwa, kupewa vifaa vya shule na makazi na asasi ya Peace Maker for Albinisim and Community, inawahifadhi wenye ualbino 35 kwenye makazi yao mkoani Arusha wakiishi pamoja na Martha eneo la Njiro.

### UJUMBE WA MALEZI

Martha anatoa ujumbe kwa wote, akirejea maisha yake asema unapomlea mtoto mwenye ualbino daima mtie moyo. Usimdhalilishe wala kumnyanyapaa. Si vyema kumwambia huwezi kufanya jambo fulani, una kasoro hii au ile kutokana na ngozi yake.

Anasema wazazi, walezi na jamii isifanye hivyo kwa kuwa mwenye ualbino ni binadamu wa kawaida.

Anatoa mfano wanafunzi wakiwa shuleni wanapojifunza mathalani mapishi, wapo walimu wanawaambia wenye ualbino wasipike kwa sababu ya joto kali wanaweza kuunga na ni hatari kwa ngozi yao.

"Haipendezi. Mwambie ajifunze mtie moyo, kama ni kuoka mikate mpe jiko mbadala asifanyekazi kwenye tanuru na joto kali. Akae sehemu yenye hewa. Tafuta maarifa ya kumwelimisha, kumpa ujuzi na stadi za maisha si kumkataza kwa kigezo cha ngozi yake."

Anataja mfano mwingine wa kushona, wapo walimu kwenye vyuo vya mafunzo wanawakataa wenye ualbino kwa kigezo kuwa wana uoni hafifu na hawawezi, anasema ni kuwakosea.: "Mpe vifaa saidizi kama miwani na vikuza herufi na maumbo ili aone, siyo kumnyanyapaa. La msingi ni kumtia moyo.

Anashauri kuepuka ubaguzi na unyanyapaa wowote iwe nyumbani au shuleni wa kuonyesha kuwa mwenye ulemavu akiwa anayeishi na ualbino wana upungufu. Anasema watoto waelimishwe kuwa wote wako sawa tofauti ni ngozi pekee, kuwa yao inakosa rangi ya asili.

### KUFAHAMISHWA ATHARI

Martha anasema wenye ualbino wanahitaji kutumia dawa au mafuta maalumu ya kulinda ngozi na athari za jua kali, ni vyema kuwaeleza watoto umuhimu wa mafuta hayo na athari za kuyaacha wakati wa malezi. Kuhusu mavazi ni vyema kuwaambia kuhusu kuvaa mavazi ya kufunika mwili, kofia na miwani kulinda macho na uso. Yote yafanywe pamoja na kubainisha athari za kuyapuuza.

### MILA POTOFU

"Wenye ualbino wanaathiriwa na mila potofu. Utasikia hawafi wanatoweka au kupotea kimaajabu. Wengine wanaamini wakijamiiana nao magonjwa yao yataondoka na kuna wanaowinda viungo vyao kwa imani ya kupata utajiri na kuwaeleza kuhusu madai ya kuwadhuru ili kupata viungo vyao. Ni vyema kuwaeleza usiwafiche."

Mlezi huyu wa wanaoishi na ualbino anasema katika malezi ni vyema kuwaeleza watoto kwa hatua kuwa wanahitaji vifaa saidizi ili kumudu maisha. Mfano miwani kusoma, kukaa mbele karibu na ubao, kutumia vikuza herufi na maumbo wakati wa kusoma na pia miavuli wanapotembea kwenye jua kali.

### JUHUDI KITAIFA

Martha anasema yaliyompata maishani hasa ututotoni yamemwamsha kufanya juhudi za kipekee kusaidia wenye ualbino kwa mfano kufundisha wakunga, wauguzi na madaktari katika mikoa mingi mijini na vijijini kufahamu chanzo cha ualbino na namna ya kuwafariji wazazi wanaojifungua watoto wenye ualbino.

*ITAENDELEA...*

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Waundwa mkakati kuwawezesha wafanyakazi, waajiri kujitambua



Ofisa wa ActionAid, Jovina Nawezake (mwenye kipaza sauti), akizungumzia kazi zenye staha na kuzingatia sheria za kazi kwenye jukwaa la kitaifa lililojadili mustakabali wa ajira nchini. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

CHANGAMOTO za wafanyakazi kutozifahamu haki zao pamoja na masuala ya kupuuza sheria kazini, ni miongoni mwa mambo yanayoifanya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kuanzisha dawati la kupokea malalamiko yanayohusu kazi na ajira.

Pamoja na kuwapo dawati hilo, wizara inalenga kuelimisha umma kuhusu haki za wafanyakazi na wajibu wa waajiri, ili waajiriwa wafahamu stahiki zao na waliowaajiri kufuata sheria na taratibu za kazi.

Ofisa Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Fred Nyaupumbwe, anasema hayo hivi karibuni kwamba lengo ni kusaidia wafanyakazi kujua na kutumia dawati hilo na pia kufahamu haki zao, kufanya kazi zenye staha na waajiri kufuata sheria za kazi.

Anasema lengo ni kuhamasisha na kuelimisha wafanyakazi kuhusu Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini pamoja na taratibu za kupata vibali vya kazi kwa wageni wanaoomba kazi nchini, kwa upande wa waajiri.

Ofisa huyo anatoa maelezo hayo kwa maofisa kazi, wafanyakazi kutoka sehemu mbalimbali na wawakilishi wa wafanyakazi kutoka Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) katika mjadala wa kitaifa kuhusu kazi za staha uliondaliwa na Shirika la ActionAid Tanzania.

Anasema uelimishaji utafanywa kupitia vyombo vya habari na uelimishaji umma kuhusu dawati la kupokea malalamiko yanayohusu kazi na ajira katika wizara hiyo.

Aidha, anawaambia washiriki kuwa wafanyakazi ndiyo wahusika wakuu na kuwataka watoe taarifa kuhusu changamoto zao iwapo maofisa kazi kutoka idara ya kazi watakwenda kukagua sehemu za kazi.

"Ili kusaidia wafanyakazi kuwasilisha malalamiko yao, idara ya kazi imetoa namba maalumu ya kutuma au kuwasilisha dukuduku kupitia namba 0655 49489 pamoja na kutuma malalamiko yao kwenye tovuti au anwania ya barua pepe ps@kazi.go.tz" anasema.

Nyaupumbwe anawaambia washiriki kuwa wameamua kujikita katika eneo hilo baada ya kugundua kuwa waajiri na watumishi wengi hawana uelewa wa sheria ya kazi wakati wafanyakazi hawafahamu haki zao katika maeneo yao na kuwahimiza kutumia fursa hiyo ili waweze kufanya kazi katika mazingira bora, kazi zenye staha na kujua haki zao.

Ofisa Kazi kutoka Idara ya Kazi Mkoa wa Pwani, Richard Muhenga, anasema, asilimia kubwa ya waajiriwa na waajiri kwenye sekta binafsi hawana elimu ya kutosha kuhusu sheria ya kazi na uhusiano kazini na hii inasababisha kuwapo migogoro katika maeneo ya kazi.

Mbali na hilo, ingawa maofisa kazi wamekuwa wakitembelea katika maeneo mbalimbali ili kufanya ukaguzi viwandani na kwenye kampuni ili kujua changamoto zinazowakabili wafanyakazi, wengi wanaogopa kutoa taarifa sahihi kuhusu matatizo yanazowakabili katika maeneo ya kazi kwa sababu wanaogopa vitisho na kufukuzwa.

"Tunaomba ofisa kazi anapofika kwenye ukaguzi toeni taarifa sahihi, msiogope kufukuzwa kazi ili tujue changamoto zinazowakabili, tuweze kuzitatua na hatimaye mfanya kazi zenye staha," anasema na kuongeza kuwa yote hayo yatafanikiwa kwa kuzingatia sheria na kuheshimu taratibu.

Akizungumzia wawekezaji wanaotoka nje, anawataka kuwasiliana na mamlaka zote zinazohusika bila kutumia mawakala na kuwakumbusha maeneo ya kuwasiliana ni pamoja na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (TIC).

Mamlaka nyingine ni ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA), Idara za Uhamiaji, Kazi , TRA pamoja na mamlaka za halmashauri sehemu anayotaka kuwekeza. "Lengo ni kuepusha usumbufu na migogoro baina ya wafanyakazi, waajiri na serikali,"anasema.

Mkuu wa Programu na Sera wa ActionAid, Jovina Nawenzake, akizungumzia suala la kazi zenye staha, anasema ni wajibu wa maofisa kazi kuhakikisha kuwa katika maeneo yao ya kazi au wilaya zao kuna kazi za staha na pia kusaidia wafanyakazi kupata stahiki zao bila kujali anafanya kazi wapi .

"Maofisa kazi mwangalie namna gani suala hili litaweza kufanyika katika maeneo yenu kwa sababu wafanyakazi wengi wanapata shida kazini kama halitatimizika basi muangalie mtafanyaje ukizingatia sasa taifa limekuwa Tanzania ya viwanda na masuala ya dijitali yamekuwa yakihusisha uvunjwaji wa haki za watu na kwamba utaongezeka kadri mabadiliko yanavyoongezeka pia," anasema.

Mbali na hilo, anawaambia wahakikishe kuwa wanaweka mikakati ili watu wafanye kazi zenye kulinda utu wao, heshima na wanapata haki zao na mafao yenye tija akisema ni jambo hilo ni mtambuka, linahitaji ushirikiano kutoka serikalini na sekta binafsi na kuishauri serikali kuweka mazingira mazuri ya wafanyakazi ili kufanya kazi zenye staha na katika mazingira bora, anakumbusha ofisa huyo.

"ActionAid Tanzania imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ili kusaidia waajiriwa kufanya kazi zenye staha, pia tunaangalia sera mbalimbali za kuisaidia serikali kupata mapato au kukosa mapato ikiwamo kodi na tunatoa mapendekezo yetu namna gani ya kuboresha sera hizo ziboreshwe ili serikali iweze kupata mapato," anasema Jovina.

Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Jordan University College- Morogoro, Asifiwe Alinanuswe, anasema kuwa maofisa kazi wafanye ukaguzi katika maeneo ya kazi ikiwamo sekta rasmi na isiyo rasmi kwa sababu huko ndipo kuna unyanyasaji mkubwa na haki za wafanyakazi kwani waajiri hazifuati. Tatizo hili tumelibaini kutokana na kesi tunazozipata katika ofisi zetu ukiwamo ukiukwaji wa vipengele vya mikataba, upungufu wa stahiki za kazi, kufukuzwa kazi bila kufuata utaratibu wa sheria za kazi na masuala mengine mengi.

Anasema: "Maofisa kazi dumisheni utu, heshima na haki za wafanyakazi kwa sababu wafanyakazi wengi katika maeneo ya kazi wanachangamoto nyingi sana, kumbukeni haki za wafanyakazi zinapatikana kwa sheria, washaurini waajiri iwapo wanakiuka sheria."

Wakizungumzia changamoto zinazowakabili vijana katika maeneo ya kazi wanasema rushwa ya ngono, kukosa elimu kuhusu mifuko ya hifadhi, mshahara midogo inayochelewa,kukosa mafao ya wafanyakazi, kutofanyika ukaguzi maeneo ya kazi, ubaguzi kazini , wafanyakazi kutoruhusiwa kujiunga na vyama vya wafanyakazi, kukosa likizo na stahiki za uzazi ni baadhi ya changamoto zinazowakabili katika maeneo ya kazi.

Wanasema changamoto hizo walizibaini baada ya kufanya utafiti na kwamba waajiri wengi hawaruhusu wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi kwa hofu kuwa watajua haki zao na baadae watadai na kupata fidia zao.

Vijana hao wanawaomba maofisa kazi kabla hawajakwenda kukukutana na waajiri, waanzie kwa wafanyakazi kwani ndiyo waonapata matatizo kazini yanayotokana na uvunjwaji wa sheria.





# Kampuni ya simu itakayotoa taarifa za mteja kushughulikiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema itaichukulia hatua kali za kisheria kampuni yoyote ya simu itakayolalamikiwa kutoa taarifa za wateja.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa katika utiaji saini wa mikataba ya kupeleka mawasiliano vijijini awamu ya tano.

Alisema wizara hiyo itahakikisha inatunga sheria ya kuwalinda wateja wa simu za mkononi ili kuondoa tabia hiyo ya kutoa siri za wateja.

Alisema, kumekuwa na malalamiko kwamba kampuni za simu za mkononi zinatoa siri za wateja jambo alilosema sio sahihi kwa mujibu wa sheria ya kampuni hizo.

"Kumeanza kuzuka wimbi katika kampuni ya simu za mkononi kutoa siri za wateja, kitendo hiki ni kinyume cha sheria na kampuni itakayobainika watumishi wake kufanya hivyo, kampuni hiyo itachukuliwa hatua," alisema.

Alizitaka kampuni hizo kusoma sheria na kuielewa na kufanya kazi kwa mujibu wa sheria huku akisema wapo watu mahsusi wanaoweza kupewa taarifa za mteja kwa mujibu wa sheria hiyo na siyo kila mtu.

Aliutaka Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), kupeleka mawasiliano katika maeneo yote nchini hasa ya mipakani ili nchi iondokane na kutumia mitandao ya nchi jirani.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, alisema kuwa katika mradi huo wa mawasiliano vijijini awamu ya tano jumla ya kata 61 zenye vijiji 173 na wakazi 728,840 zitafikishiwa mawasiliano ya simu.

# Serikali yazionya shule binafsi kukaririsha wanafunzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekemea tabia ya baadhi ya shule zisizo za serikali kwenda kinyume na maelekezo ya serikali ikiwamo kumkaririsha mwanafunzi darasa licha ya kufaulu mitihani ya kitaifa.

Mwaka 2018, serikali ilitoa Waraka wa Elimu namba mbili ambao ulielekeza utaratibu mpya wa kukariri darasa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari baada ya wazazi kulalamikia kitendo hicho.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa wakuu wa shule za sekondari na msingi za makanisa, ulioratibiwa na Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC).

"Tunatambua mchango wenu mnaoutoa nchini katika sekta ya elimu, hata hivyo, baadhi ya shule zisizo za serikali kama nyingine zipo kwenu au hazipo, ambazo zinaenda kinyume na maelekezo ya serikali, niwakumbushe myazingatie kukaririsha wanafunzi bila kuzingatia taratibu ni tatizo tunalokutana nalo sana," alisema.

Alisema tatizo la kukaririsha wanafunzi usiozingatia taratibu limekuwa likijitokeza mara kwa mara.

"Kuna mifano ya kulazimisha wazazi wakubali watoto wao warudie darasa hata kama amefaulu mitihani ya taifa ya upimaji wa darasa la nne na kidato cha pili," alisema.

Aliwataka kufuata taratibu zilizowekwa katika eneo hilo kwa kuwa zipo bayana.

Alisema serikali imepokea malalamiko ya kutofuatwa kwa ratiba za uendeshaji wa shule.

"Kuna baadhi ya shule tena zina watoto wadogo wapo bweni wanaamshwa asubuhi sana tena saa 11 alfajiri kulingana na ratiba za shule, sijui wawahi mitihani yao ya saa moja, kabla ya masomo, wanaamshwa mapema wanachoka, tuangalie ratiba ambazo wizara imetoa na zinashauriwa kitaalamu," alisema.

Alisema watoto wa sasa hawapati muda wa kucheza kutokana na ratiba za shule kubanwa. "Vilevile, kuna taarifa watoto ambao sio wa bweni wanalazimishwa kufika shule saa 12 asubuhi, hata usafiri wa kuwafikisha utaupata wapi, ratiba hizi zinaleta usumbufu kwa wanafunzi na hata wazazi," alisema.

Kuhusu ombi la kupunguza mitihani ya majaribio lililotolewa na Tume hiyo, Katibu Mkuu huyo alikiri kuwa suala hilo lina utata na kudai kuwa ni mingi na wakati mwingine inaipa wizara wakati mgumu kuiratibu.

"Kuna wengine wanadhani elimu inapatikana kwa kuuliza wanafunzi maswali mara kwa mara, ili ng'ombe anenepe ni kuhakikisha amekula na si kumpima uzito asubuhi, mchana na jioni, kitu kizuri ni kuimarisha ufundishaji," alisema.

"Kuna dhana nyingine imeongezeka hadi kuweka kambi kufanyishwa mitihani kila siku hadi Jumamosi, kuna mambo tumekemea na si sahihi kwamba ili mwanafunzi afaulu ni kufanya mitihani, majaribio hatuyakatai bali kila mara inamchosha mtoto." Vile vile, alisema nia ya serikali ni kutoleta mgongano na wanaendelea na majadiliano na kutaka kuimarisha ufundishaji na si kupewa mitihani kila siku.

Dk. Akwilapo alizishukuru shule hizo za makanisa kwa kusaidia kutoa huduma ya elimu kwa jamii.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Tume hiyo, Peter Maduki, alisema lengo la mkutano huo ni kuweka mikakati ya utoaji huduma bora ya elimu na kuangalia kero zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi.

"Pia tutajadili namna ya kuboresha huduma ya TEHAMA itatusaidia sana katika kuboresha elimu na kupunguza gharama ya utoaji wa elimu na kuwapunguzia mzigo wazazi," alisema.

Aliomba wizara kuangalia namna ya kupunguza mitihani ya majaribio ambayo imeonekana kuendelea kuibuka mbali na inayopaswa kufanyika kitaifa.

"Kunaendelea kuibuka mitihani ya majaribio mara ya kikata, kiwilaya hali inayosababisha mwingiliano wa mitihani na hii hata inashusha ubora wa mitihani tunaomba umakini zaidi uwepo katika kuendesha mitihani," alisema.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Humphrey Polepole (kushoto), akiongoza kikao cha kamati hiyo, bungeni jijini Dodoma jana. Kamati mbalimbali za Bunge zinaendelea na vikao vyake kabla ya kuanza kwa Bunge wiki ijayo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Waomba kujengewa daraja Godegode

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANANCHI wa Kata za Kusini mwa Jimbo la Mpwapwa mkoani hapa, wameomba serikali kuwajengea daraja la Godegode lililosombwa na mvua miaka miwili iliyopita.

Kusombwa kwa daraja hilo, kunawalazimu kuvushwa kwa kubebwa mgongoni na vijana kwa gharama kati ya Sh. 6,000.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi hao walisema kata zinazopata kero hiyo ni Godegode, Pwaga na Lumuma.

Mmoja wa wananchi hao, Samwel Chinyele, alisema serikali iliahidi kulijenga, lakini hadi sasa halijajengwa daraja hilo na wakati wa mvua ndiyo kero kwao kwa kuwa mtu anapotaka kuvuka upande wa pili analazimika kubebwa mgongoni kutokana na wingi wa maji.

Akizungumzia hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alikiri kuwapo kwa adha hiyo kwa wananchi huku akisema serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS), ililazimika kufanya usanifu wa daraja jipya kwa kuzingatia kupanuka kwa Bonde la Mto Chinyasungu linalovuna maji kutoka maeneo mengine ya nchi.

"Tayari usanifu wa kina umefanyika, pia tayari ujenzi wake umeingizwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kwa hiyo lipo kwenye hatua nzuri sasa kutengewa fedha na kujengwa," alisema.

# Bil. 3.5/- kutatua tatizo sugu la maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

ZAIDI ya Sh. bilioni 3.5 zinahitajika kwa ajili ya kutatua tatizo sugu la uhaba wa maji katika miji ya Kyela na Kasumulu, wilayani Kyela.

Wakazi wa miji hiyo wamekuwa wakihangaika kupata huduma hiyo kutokana na kukosa chanzo cha uhakika cha maji ya kutosheleza ambayo ina watu wengi na imekuwa ikikumbwa na magonjwa yanayotokana na matumizi ya maji machafu.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA), imefanya utafiti na kufanikiwa kupata chanzo kipya cha maji kinachopatikana ndani ya Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Ndele Mengo, alisema chanzo hicho ni cha uhakika na kina uwezo wa kuhudumia miji hiyo pamoja na vijiji vinavyozunguka chanzo hicho.

Alisema kwa sasa wanatafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na endapo watapata fedha hizo kutoka Serikali Kuu wataukamilisha mradi ndani ya miezi 18 ijayo na wananchi kuanza kupata huduma.

"Haya maji ni safi na ni mengi sana, chanzo kipo na kilishajengwa miaka kadhaa iliyopita na sasa hivi kinahitajika tu kuboreshwa na kuanza kupeleka maji kwa wananchi," alisema Mengo.

Alisema walishafanya usanifu na kujiridhisha kuwa chanzo hicho kinakidhi mahitaji ya wananchi wa miji hiyo miwili kwa miaka zaidi ya 20 na wataendelea kutafuta vyanzo vingine.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Mlaghila, alisema mradi huo ni muhimu kwa ajili ya kukabili tatizo la maji kwenye jimbo hilo kwa maelezo kuwa tatizo kubwa la wilaya hiyo ni maji.

Alisema wananchi wanatumia muda mrefu kutafuta huduma hiyo kwenye mito na visima ambavyo wakati mwingine usalama wake sio wa uhakika.

"Sisi wana Kyela tatizo kubwa linalotukabili ni maji, tunawaomba watu wa mamlaka mtusaidie kukamilisha mradi huu mapema ili tuondokane na tatizo hili," alisema Mlaghila.

Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kyela, walisema wamekuwa wakikumbwa na magonjwa ya milipuko na kuhara kutokana na maji wanayotumia kuwa na vijidudu.



Baadhi ya wasichana wenye umri wa kuanzia miaka 18- 35 kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Kyela akiwamo Shukuru Mwakamala (anayezungumza) wakieleza shughuli mbalimbali za ujasiriamali wanazozifanya ili kujikwamua kiuchumi, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yanayoendeshwa na Taasisi ya Tanzania Data Lab (Dlab) kupitia programu ya Data4Her kwa kushirikiana na ufadhili wa Shirika la PEPFAR jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA** .

# 'Wenye ulemavu wapewe mafunzo usalama kazini'

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI imesema iko haja ya kuwawezesha watu wenye ulemavu katika shughuli za uzalishaji kupitia mafunzo ya usalama na afya kazini na kuwapa mitaji ili wawaze kuboresha shughuli zao za kiuchumi.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kukuza uelewa wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi yalioandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA), Mkoa wa Mbeya.

"Serikali imeamua kutoa mafunzo ya usalama na afya kwa makundi mbalimbali ili waweze kuepukana na madhara yanayoweza kusababishwa na kutozingatia kanuni za usalama na afya kazini," alisema.

Alitoa pongezi kwa OSHA kwa kutekeleza ipasavyo wajibu wake ikiwamo kufanya ukaguzi wa usalama na afya katika sehemu nyingi za kazi pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala ya afya na usalama kazini na kuitaka kuongeza jitihada zaidi ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mafunzo hayo ya siku moja yalijikita katika kuainisha na kushauri mbinu za kudhibiti vihatarishi vya usalama na afya ambavyo huambatana na shughuli mbalimbali za uzalishaji ikiwamo ujenzi, kilimo, ufundi seremala, kilimo, ufugaji, biashara ndogondogo pamoja na kazi za ofisini.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mafunzo hayo yanatolewa kwa makundi mbalimbali ya kijamii wakiwamo watu wenye ulemavu katika mikoa mbalimbali na kusisitiza mafunzo hayo ni endelevu.

"Kama taasisi yenye dhamana ya usalama na afya kwa mfanyakazi, tumeona kuna umuhimu wa kuyafikia makundi haya ya watu wenye ulemavu kwa kuwa tunatambua kwamba ulemavu ni hali tu na haupaswi kuwa kikwazo kwa mtu kushiriki katika shughuli za kiuzalishaji," alisema.

"Tumeshayafikia makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu katika mikoa kadhaa ukiwamo Kagera, Dar es Salaam, Pwani na sasa Mbeya na tutaendelea kutoa mafunzo haya katika mikoa mingine," alisema Mwenda.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Renatha Exsavery, mwanafunzi wa ufundi katika Chuo cha VETA mkoani humo, alisema amefurahishwa na mafunzo hayo na yatawawezesha kujilinda dhidi ya vihatarishi mbalimbali vilivyopo katika sehemu zao za kazi.

# Wanufaika elimu upangaji bajeti mrengo kijinsia

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

BAADHI ya wakulima na wafugaji wa Kijiji cha Shibolya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameanza kunufaika na elimu ya upangaji bajeti yenye mrengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia iliyotolewa na shirika lisilo la kiserikali la Elimisha.

Mmoja wa wafugaji waliopata elimu hiyo, Rehema Nsolo, alisema wanawake hawajapewa kipaumbele kushirikishwa kwenye utoaji wa uamuzi, jambo linalosababisha familia nyingi kutokuwa na bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Nsolo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika Kijiji cha Shilolya, wakati Shirika la Elimisha likitoa elimu ya upangaji bajeti yenye mrengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia uliokuwa na lengo la kuweka usawa katika matumizi ya rasilimali fedha.

Alisema wanawake wengi wanajukumu la kuhakikisha mazao na mifugo yanakuwa salama, lakini unapofika muda wa mauzo wanaume ndiyo wanahusika na shughuli zote za uuzaji na kupanga matumizi ya fedha hizo bila kuwahusisha wake zao.

"Asilimia 80 ya wanawake vijijini ndiyo wazalishaji, lakini wengi hatuna maamuzi wakati wa mauzo ya tulichozalisha, elimu hii imetusaidia kutambua haki zetu hivyo ni wakati wetu kupigania bajeti yenye mlengo wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia," alisema Nsolo.

Aliwataka wanawake wote wanaojihusisha na kilimo pamoja na ufugaji kuhakikisha hawako nyuma unapofika wakati wa mavuno na upangaji wa bajeti kushiriki kama wazalishaji wakubwa badala ya kuwaachia wanaume ambao wakati mwingine fedha za mavuno huzitumia kuhonga michepuko na ulevi.

Akieleza lengo la utoaji wa elimu hiyo, Festo Sikagonamo, alisema upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia utasaidia kupunguza vichocheo vya umaskini kwenye jamii, wizi, rushwa, kuongeza ufanisi wa kazi na kuwafanya watu kuwa na matumizi yanayoendana na kipato.

Alisema upangaji huo wa bajeti utasaidia kufahamu unatumia shilingi ngapi kwa siku, shughuli unayoifanya ikuingizie shilingi ngapi ili uweze kukidhi mahitaji yako.



# Bodi ya Vileo yatakiwa kung'oka

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa Bodi ya Udhibiti na Ushauri wa Vileo Zanzibar wametakiwa kujiuzulu baada ya kutoa vibali kwa kampuni sita kuingiza pombe badala ya tatu kwa mujibu wa sheria mpya namba 9 ya mwaka 2020.

Wito huo ulitolewa na wanaharakati wa haki za binadamu na wanasheria walipokuwa wakizungumzia mgogoro wa sheria namba 9 ya mwaka 2020 baada ya kuanza kutumika Januari mwaka huu na kusababisha mfumuko wa bei ya vileo Zanzibar.

Wakili maarufu Zanzibar, Rajab Abdallah, alisema kwa mujibu wa kifungu cha 33 (1) kimeeleza kibali cha kuingiza vileo kitatolewa kwa waangizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia masharti kwanza mhusika awe Mzanzibari, awe mlipakodi, awe na ghala la kuhifadhia pamoja na gari maalum la kusambaza vinywaji vyake.

"Kitendo cha kuweka kando sheria na kutoa vibali kwa kampuni sita badala ya tatu ni uvunjaji wa sheria na Mwenyekiti wa Bodi anapaswa kujiuzulu kwa kuvunja sheria," alisema Wakili Rajabu.

Alisema Zanzibar inaongozwa kwa misingi ya utawala wa sheria na hakuwa mwafaka kwa Mwenyekiti wa Bodi kutumia hekima na busara kuongeza idadi ya kampuni kwa madhumuni ya kulinda maslahi mapana ya serikali ya kukusanya kodi.

Rajab alisema kabla ya sheria kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais wa Zanzibar Mei mwaka 2020 mapendekezo ya sheria yalijadiliwa na wadau wa vileo, makatibu wakuu pamoja na Baraza la Mawaziri kabla ya muswada wa sheria kupelekwa barazani.

"Mwenyekiti wa Bodi anataka kutuambia viongozi wote waliojadili sheria hii wakiwamo makatibu wakuu, wawakilishi na Baraza la Mawaziri wakiongozwa na rais hawakuona maslahi mapana ya mapato ya serikali mpaka wakaweka ugomo wa idadi ya kampuni za kuingiza pombe mwisho tatu kwa mujibu wa sheria," alihoji Wakili Rajabu.

Alisema kampuni zote zilizopewa vibali vya ziada zitakuwa zinafanya biashara kinyume cha sheria kwa vile vibali walivyopewa sawa na karatasi kwa sababu vimetolewa kinyume cha sheria.

Kwa upande wake Mwanaharakati wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Makame Issa, alisema maamuzi yaliyofanywa na Bodi ya Vileo yanakwenda kinyume cha misingi ya utawala bora.

"Nchi inaongozwa kwa kufuata katiba na sheria, sio hekima na busara ndio maana kunatungwa sheria na hakuna mamlaka yoyote yenye ubavu wa kuvunja sheria," alisema Issa.

Alisema kama kutafuta mapato serikali ingelikuwa na uwezo wa kuuza dawa za kulevya au kutakatisha fedha, lakini haiwezi kufanya hivyo kwa sababu ni kinyume cha sheria.

Hata hivyo, alipoulizwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji, kuhusu mvutano wa vibali vya kampuni za uingizaji wa vileo hakutaka kuzungumza chochote.

Mwenyekiti wa Bodi ya Udhibiti na Ushauri ya Vileo Zanzibar, Abdulrazaki Abdulkadiri, alisema mtu yeyote ambaye anaona sheria imevunjwa yuko huru kwenda mahakamani.

"Bodi kweli tumeongeza kampuni zaidi ya tatu kwa baada ya kuzingatia maslahi mapana ya serikali katika ukusanyaji wa mapato na kampuni ambazo zilikuwa zimekosa ni walipaji wakubwa wa kodi kupitia vileo," alisema.

Naye Kiongozi Mwandamizi wa Taasisi ya Kiislamu Zanzibar, Sheikh Abdalla Hussen, alisema malengo ya kutungwa sheria mpya ya vileo imelenga kudhibiti biashara ya pombe kufanyika kiholela katika mitaa pamoja na maeneo ya huduma za jamii.

Alisema bodi inapaswa kuchunguzwa kutokana na maamuzi waliyofanya kutokana na kuvunja sheria kinyume cha madhumuni ya kutungwa sheria ya kudhibiti na kusimamia vileo.



Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka, akikabidhi TV kwa wagonjwa waliolazwa wodi ya mifupa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, jana. **PICHA: OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MJINI**

# Waziri awashauri wanaharakati vijana

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, amewasisitiza wanaharakati vijana kushirikiana na serikali katika kusaidia kuielimisha jamii.

Tabia alitoa msisitizo huo wakati wa hafla ya kuwatunuku vijana Tuzo za Zanzibar Youth Award msimu wa pili, juzi usiku.

Alisema kupitia harakati ambazo vijana hao wanajishughulisha nazo, wanaweza kutoa mchango mkubwa katika kuishawishi jamii kuondokana na matatizo mbalimbali yanayorudisha nyuma maendeleo ya Taifa, ikiwamo suala la dawa za kulevya.

Alisema Zanzibar ina vijana wengi wenye uwezo, uthubutu na vipaji ambavyo vikiendelezwa na kutumika vizuri vinaweza kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ndani ya jamii.

Aidha, aliwataka vijana hao kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa Baraza la Vijana unaotarajiwa kufanyika karibuni, ili kupata fursa ya kuisaidia serikali katika kutunga sera na sheria zinazowasimamia vijana.

Tabia aliahidi kutoa ushirikiano kwa Taasisi ya Zanzibar Youth Talk katika kuuwezesha mradi wa Zanzibar Youth Award kupata ufadhili wa serikali.

Aliwaahidi kuwa atashirikiana na taasisi hiyo katika kuifufua Zanzibar Music Award ili iweze kuwahamasisha vijana kukuza vipaji vyao jambo ambalo litawasaidia kupata fursa za kujiajiri wenyewe.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Zanzibar Youth Talk, Farida Nassor Moh'd, amesema lengo la taasisi hiyo ni kuhakikisha wanapaza sauti za vijana pamoja na kusaidia kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili.

# Kaskazini watakiwa kuchukua tahadhari za majanga mapema

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Aboud Hassan Mwinyi, amewataka wananchi kuchukua tahadhari mapema za kukabiliana na maafa ikiwamo mvua zinazonyesha mara kwa mara kuepukana na athari za kutuama maji katika maeneo yao.

Mkuu wa Wilaya alitoa wito huo katika Kijiji cha Matetema Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja alipokuwa akikabidhi msaada wa chakula kwa wananchi waliopatwa na maafa wakati wa kipindi cha mvua zilizopita hivi karibuni.

Msaada huo wa vyakula ulitolewa na Shirika la Mwezi Mwekundu la Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu.

Alisema lengo la serikali ni kuwasaidia wananchi wake pale wanapopatwa na majanga ila ni vyema wananchi wakachukua tahadhari mapema ili kujiepusha kupatwa na majanga, na sio kusubiri kupatwa na maafa kwa ajili ya kusaidiwa na serikali.

"Wananchi mnapaswa kuchukua tahadhari kabla ya kusubiri hatari, mara nyingi mvua zinapokaribia mamlaka zetu za hali ya hewa huwa zinatoa taarifa ya mvua hizo, hivyo ni vyema kuzizingatia taarifa zinazotolewa na mamlaka husika ili kujiepusha na maafa zaidi," alisema.

Alisema wananchi wanaoishi maeneo ya mabondeni na yanayotuama maji katika vipindi vya mvua kubwa ni vyema wakaondoka maeneo hayo kwa wakati sahihi badala ya kusubiri mvua kunyesha hali inayoleta athari nyingi.

Aidha, alisema katika kukabiliana na maafa ya mafuriko wilaya kwa kushirikiana na Serikali Kuu imeshaweka mipango mizuri ya ujenzi wa makazi kwa kufuata taratibu za mipango miji katika miji midogo ya maeneo ya vijijini.

Naye Sheha wa Shehia ya Matetema, Mohammed Bakar, alisema pamoja na kuwa baadhi ya watu hupata maafa kwa kujenga maeneo ya mabondeni au kuwa karibu na mito maafa mengine husababishwa na ujenzi wa miundombinu.

Alisema ujenzi wa barabara kuu umewaathiri kwa kiasi kikubwa baadhi ya wananchi wa kijiji hicho kwa nyumba zao kuingiliwa na maji mvua zinaponyesha kwa baadhi ya barabara kutotolewa mitaro ya kupitishia maji, hali inayosababisha maji kuingia katika nyumba za watu.

Nao wananchi wa Shehia ya Matetema wameushukuru uongozi wa Wilaya ya Kaskazini 'B' kwa kuwapatia msaada wa vyakula kwa kukumbwa na maafa ambapo walisema msaada huo utawasaidia katika kipindi hiki ambapo mazao yao bado hawajaanza kuvuna kwa kula na hata biashara.

# Kimbunga Eloise, mafuriko vyaua watu 10 Msumbiji

**Beira, MSUMBIJI**

KIMBUNGA Eloise kilichotokea katika mji wa Beira, kimesababisha vifo vya watu 10, nchini Msumbiji.

Watu hao walifariki dunia baada ya kimbunga hicho kupiga pwani ya Mashariki mwa Afrika na kusababisha mvua mkubwa iliyoambatana na upepo mkali kasi ya kilometa 160 kwa saa.

Kulingana na maofisa wa serikali ya Msumbiji, vifo vingi vimeripotiwa kwenye mji wa Bandari wa Beira baada ya kuangukiwa na miti.

Wilaya za Buzi na Nhamatanda pia zimeathiriwa na mafuriko, yaliyotokana na kimbunga hicho.

Hata hivyo nguvu ya kimbunga hicho imepungua wakati kikielekea nchi jirani ya Zimbabwe, Botswana na baadhi ya maeneo ya Afrika Kusini.

Nchini Madagascar, taifa ambalo kimbunga hicho kilianzia, maofisa walisema mtu mmoja alifariki dunia na kumeshuhudiwa pia mafuriko.

Beira ilipata milimita 250 za mvua katika kipindi cha saa 24, kulingana na taasisi ya kitaifa ya hali ya hewa nchini humo, INAM. Baadhi ya maofisa na mashirika ya misaada yanachunguza kiwango cha uharibifu huo, ili kuweza kuwasaidia walioathirika na kujaribu kurudisha umeme na mawasiliano katika baadhi ya maeneo.

Watu waliuawa kulingana na maofisa.

Chris Neeson, ambaye anafanya kazi katika Umoja wa Mataifa (UN) katika mji wa Beira alisema, ilikuwa vigumu kulala kutokana na kelele na hofu.

"Nilisikia upepo mwingi na mvua ikinyesha mapema alfajiri.

"Maji yaliingia katika nyumba yangu, pamoja na mawe na majani ambayo yalikuwa yametoka katika nyumba za majirani zangu.

"Umeme ulikatika tangu usiku uliopita na tumeshindwa kupiga simu."

Wakazi wa Beira, mji wa pili kwa ukubwa nchini Msumbiji una idadi ya watu wapatao 500,000, wanajaribu kuusafisha mji huo.

Zaidi ya nyumba 1,000 zimeharibiwa na nyingine 3,000 zikiharibiwa vibaya kulingana na Antonio Beleza, kutoka taasisi ya usimamizi wa majanga.

Alisema kwamba zaidi ya watu 160,000 waliathiriwa moja kwa moja.

Baadhi yao wanajaribu kuokoa chochote kutoka katika nyumba zao zilizokumbwa na mafuriko, huku miti, nyaya za umeme pamoja na mabango ya matangazo yakisombwa na upepo.

Baadhi ya mito katika eneo hilo pia imevunja kingo zake.

Eneo hilo lilikuwa pia na vimbunga viwili, ikiwamo kimbunga Idai na Kenneth, ambavyo viliikumba nchi hiyo, mwaka 2019 na kuua mamia na maelfu wakiachwa bila makazi.

*DW/BBC*



Nyumba ikiwa imezingirwa na maji katika mji wa Beira, uliokumbwa na kimbunga Eloise, nchini Msumbiji, kilichosababisha vifo vya watu 10 na kuathiri watu 160,000 katika pwani ya Mashariki mwa Afrika. **PICHA/BBC**

# Rais Jerry Rawlings kuzikwa kesho

**Accra, GHANA**

MAZISHI ya Rais wa zamani wa Ghana, Jerry Rawlings aliyefariki Novemba 12, mwaka jana, yanatarajia kufanyika kesho.

Taratibu za mazishi hayo zilianza tangu Januari 24, mwaka huu katika mji mkuu wa nchi hiyo, Accra.

Kulifanyika ibada ya misa ya uzinduzi, ambayo ilifungua shughuli ya mazishi ya serikali ya Jerry Rawlings.

Familia ya marehemu, ilikuwa mstari wa mbele, pamoja na Rais Nana Akufo-Addo na Kiongozi wa Chama cha Upinzani, John Mahama, kuhudhuria mahubiri yaliyotolewa na Askofu Mkuu wa Cape Coast.

Shughuli hiyo iliendelea hadi Jumatatu jioni katika makao makuu ya Jeshi la Anga. Jerry Rawlings alikuwa rubani wa ndege za kijeshi kabla ya kuchukua madaraka, mwaka 1981.

Mwili wa hayati Rawlings ulianza kuagwa Jumatatu katika mji mkuu.

Wajumbe wa serikali walifika katika Jumba la Burning kwa heshima ya mwisho kwa mkuu wa zamani wa nchi.

Wakuu wa jadi wa eneo la Anlo, alikotokea Rawlings, wiki iliyopita walitaka mwili wake kurudishwa katika mkoa wao Mashariki mwa nchi.

Walitarajia kumzika rais huyo wa zamani katika mkoa huo, kulingana na ibada zao za mazishi licha ya ombi kutotazingatiwa.

Sherehe za mazishi zitafanyika kesho katika uwanja wa Uhuru na Jerry Rawlings anatarajiwa kuzikwa katika makaburi ya Jeshi la Accra, kama wakuu wa nchi waliomtangulia.

*RFI*

# ICC yamnasa kamanda uasi wa Jamhuri ya Kati

**The Hague, UHOLANZI**

MAHAKAMA ya kimataifa ya jinai ya ICC, imesema kuwa imemtia mbaroni aliyekuwa kamanda wa kundi la uasi la Seleka, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), linaloshukiwa kutekeleza uhalifu wa vita na uhalifu dhidi ya ubinadamu.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters, ICC ilisema kuwa, Mahamat Said Abdel Kain, alijisalimisha mwishoni mwa wiki na kukamatwa kufuatia hati ya iliyotolewa Januari 7, mwaka 2019 kutokana na ukatili uliotekelezwa mwaka 2013.

Hata hivyo tarehe ya kufikishwa mahakamani mjini, Hague haijatangazwa.

Ukamataji huo umefanyika wakati kukiwa na hali ya taharuki nchini humo, kufuatia mapigano kati ya jeshi la serikali likiungwa mkono na Russia na Rwanda na waasi wanaopinga ushindi wa Rais Faustin Archange Touadera, baada ya uchaguzi wa Desemba 27.

Taifa hilo limekuwa likishuhudia machafuko tangu muungano wa waasi wa kiislamu kutoka upande wa Kaskazini uitwao, Seleka, walipochukua madaraka Machi, mwaka 2013.

Utawala wao ulisababisha wapiganaji wa kikristo kwa jina anti balaka ambao wengi wa viongozi wao wanakabiliwa na mashtaka mbele ya ICC.

*VOA*

## Korti yaamuru kutozingira nyumbani kwa Bobi Wine

**Kampala, UGANDA**

MAHAKAMA nchini Uganda, imetoa amri, jeshi na polisi kuondoka nyumbani kwa aliyekuwa mgombea urais, Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine.

Bobi Wine kwa zaidi ya siku 11 hadi jana, hajawahi kutoka nyumbani kwake, baada ya uchaguzi mkuu na kutangaza kuwa mshindi wa pili, akitanguliwa na Rais Yoweri Museveni.

Hukumu ya Mahakama Kuu, iliyotolewa siku ya jana, imekuja baada ya suala hilo kufikishwa mahakamani na mawakili wa Bobi Wine.

Serikali ilidai kuwa, ilihitaji kumzuia kwa kuwa alipanga kufanya maandamano.

Bobi Wine alidai kuwa mchakato wa kura ulikumbwa na udanganyifu.

Katika hatua nyingine, Tume ya uchaguzi nchini humo, imekanusha kuchapisha kwenye tovuti yake matokeo ya uchaguzi uliofanyika hivi karibuni, kisha kuliondoa chapisho hilo.

Tume hiyo tarehe 17 mwezi Januari, ilimtangaza Rais Yoweri Museveni kuwa mshindi kwa kupata asilimia 59 ya kura zilizopigwa.

Mgombea wa nafasi hiyo pia, Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, akipata asilimia 35 huku matokeo rasmi ya uchaguzi huo bado hayajachapishwa, tume ilisema, mwishoni mwa wiki.

Tume ilisema, imezifanyia majaribio anwani ambazo matokeo yatachapishwa.

Anwani za tovuti zilizojaribiwa ziliondoshwa, ilisema tume hiyo. "Si kweli kuwa Tume ya Uchaguzi Uganda, imefuta au kuondoa matokeo kwani matokeo rasmi hayajachapishwa.

"Matokeo yatachapishwa kwenye magazeti na tovuti," iliandika tume hiyo kwenye ukurasa wa Twitter.

*BBC*



# SOLSKJAER

## ATAJA SABABU USHINDI KWA LIVERPOOL

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema 'Mashetani Wekundu' hao walitengeneza "agano" kwa kiwango chao cha kuvutia kwenye mchezo wa ushindi wa Kombe la FA dhidi ya Liverpool.

Ushindi wa United wa mabao 3-2 pale kwenye dimba la Old Trafford ulipatikana dakika ya 78 kwa shuti la adhabu ndogo kutoka kwa mtokea benchi, Bruno Fernandes, baada ya mabao ya mapema kutoka kwa Mason Greenwood na Marcus Rashford, Jumapili.

Mabao mawili ya Mohamed Salah yaliifanya Liverpool kuwa kwenye nafasi nzuri kabla ya Fernandes kufunga bao hilo la ushindi.

"Tumepata njia ya kujiamini, wachezaji wanaamini, na tunaimarika siku hadi siku," alisema Solskjaer.

"Tunatafuta utofauti tangu mwaka mmoja uliopita au miezi sita nyuma. Jambo la msingi ni kushinda kila mchezo na hilo ndio agano letu kwa sasa.

"Ni hisia nzuri kucheza kwa kiwango cha kuvutia kwa namna hii kama tulivyopanga."

Solskjaer alisema United awali walitafuta "mifumo tofauti ya kuwamaliza wapinzani wao", lakini sasa mambo ni tofauti kabisa.

"Bila shaka, agano hili ni la kwetu wenyewe," aliongeza kusema Solskjaer. "Hilo limeimarisha kujiamini kwetu na sasa tunaweza kucheza kwa kiwango bora kwa staili yetu wenyewe."

# AGUERO ANAIPA TABU MAN CITY - GUARDIOLA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema Manchester City wapo kwenye wakati mgumu kutokana na kumkosa nyota wao Sergio Aguero ambaye anasumbuliwa na majeraha.

Aguero hakuwapo pia kwenye mchezo wa Man City wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Cheltenham Town kwenye Kombe la FA, Jumamosi.

Aguero ambaye ametumika ndani ya City kwa muda wa miaka tisa na nusu, mkataba wake unakaribia kumalizika na anatajwa kutoongeza mwingine.

Amekuwa mhimili ndani ya City akiwa amecheza jumla ya mechi 379 na kutupia mabao 256, ambapo kwa sasa anasumbuliwa na goti ambalo aliumia msimu uliopita.

Jitihada za kurejea kwenye ubora zimekuwa zikikwama kwa kuwa amecheza mechi tano pekee ndani ya City msimu huu.

Guardiola amesema kuwa anatamani kumuona Aguero akiwa uwanjani, lakini hana namna ya kufanya.

"Tumemkumbuka kwa anachokifanya na hakuna namna ambayo tunaweza kuifanya kwa sasa," alisema Guardiola akinukuliwa na Sky Sport.

"Uwezo wake unaonekana na ni moja ya washambuliaji wazuri, na tunakosa huduma yake muhimu kwa sasa."



# SIMEONE: ATLETICO INAMHITAJI SANA JOAO

**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone amesisitiza kuwa Atletico Madrid "mara zote wanamhitaji" Joao Felix licha ya mshambuliaji huyo kutokuwa kwenye kiwango kizuri wiki za hivi karibuni.

Felix alifunga bao moja na kutoa pasi ya mwisho moja wakati vinara hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Atletico walipoichapa Valencia 3-1 Jumapili, lakini ndio ulikuwa mchezo wa kwanza wa ligi kuanza kwa nyota huyo mwaka huu, ambaye aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo.

Mshambuliaji huyo wa Ureno hakufunga bao kwenye LaLiga tangu Novemba 7, kitu kilichomgharimu nafasi ya kuanza kwenye kikosi hicho cha kocha, Simeone.

Hata katika mchezo dhidi ya Valencia, alijaribu kupiga mashuti matatu na kutengeneza pasi mbili muhimu, Joao Felix alitolewa dakika ya 62 na nafasi yake kuchukuliwa na Angel Correa.

Na Correa alipoingia alifunga bao la tatu - baada ya Joao Felix kutengeneza bao la Luis Suarez na yeye kufunga.

"Joao Felix ni mchezaji wa aina yake," alisema Simeone akiwaambia waandishi wa habari. "Mara zote tunamhitaji.

"Mashindano yapo kwenye kiwango cha juu, na kila timu inasaka ushindi na kila mchezaji anataka kucheza.

"(Joao Felix) amekuwa akifanya vizuri tangu alipowasili hapa. Ni mchezaji muhimu na amejitoa kwa kila kitu kutusaidia sisi."






# FERNANDES

## AMPA NENO VAN DE BEEK

**MANCHESTER, England**

BRUNO Fernandes anaelewa kutokuwa na furaha kwa Donny van de Beek na amesema kukosa nafasi ya kucheza kwa kiungo mwenzake huyo, kunaonyesha namna gani Manchester United ina kikosi imara na kipana.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi, Van de Beek alianza kwenye mchezo wake wa 10 kwa United wakati wakishinda dhidi ya Liverpool kwenye FA, Jumapili.

Amekuwa kwenye wakati mgumu kuwa na nafasi pale Old Trafford, hata hivyo, aligusa mpira mara 23 na kutengeneza pasi 18 kabla ya kutolewa dakika ya 66.

Fernandes aliingizwa kuchukua nafasi ya Mholanzi huyo na kwa mara nyingine tena alionyesha umuhimu wake baada ya kufunga kwa shuti la adhabu ndogo na kuipa timu yake ushindi wa mabao 3-2.

Ole Gunnar Solskjaer alibainisha kwamba, Van de Beek hana furaha kwa sababu hapati nafasi ya kucheza mara kwa mara na Fernandes ametia neno lake kwa nyota huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 40.

"Donny alikuwa na mchezo mzuri," alisema akiiambia MUTV. "Kucheza nafasi ninayocheza, kumtazama namna alivyokuwa anaondoka na mpira, lilikuwa jambo zuri.

"Ni jambo muhimu kwetu sisi. Kama ningekuwa Donny nisingeonyesha kutokuwa na furaha, kwa sababu jambo la muhimu ni kufanya kile unachoweza kwa timu."

# DE JONG AMKUNA KOEMAN BARCA

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amemsifia Frenkie de Jong kwa kuimarika kwenye nafasi ya ushambuliaji baada ya kufunga bao na kutoa pasi ya mwisho wakati Barcelona wakishinda 2-0 dhidi ya Elche.

Nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi, alitumia vizuri makosa ya Diego Gonzalez kuipa Barca bao la kuongoza dakika ya 39 na alimtengenezea pande Riqui Puig aliyetokea benchi na akafunga bao la pili kwenye mchezo huo uliopigwa Jumapili.

De Jong sasa ana mabao matatu na pasi za mwisho mbili kwenye mechi sita za mashindano yote, huku mabao yake matano kwenye LaLiga kwa kipindi cha miezi 18 pale Camp Nou ni moja zaidi ya yale aliyofunga kwenye Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie alikokaa kwa misimu mitano.

"Washambuliaji watatu hawatoshi; tunahitaji viungo kufunga pia," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni jambo zuri kwamba anafunga na kutoa pasi za mwisho.

"Mara zote anazidi kuimarika. Tunataka viungo kuingia kwenye boksi la penalti na kufunga."

Barcelona itarudi kwenye mchezo mwingine Jumatano wakati watakaposafiri kwenda kucheza na Rayo Vallecano hatua ya 16-bora ya Kombe la Mfalme (Copa del Rey).



# LAMPARD AWATETEA KEPA, WERNER



**LONDON, England**

FRANK Lampard amemtetea, Kepa Arrizabalaga na amesema hana shaka Timo Werner ataendelea kuwa vizuri baada ya Chelsea kuibuka na ushindi kwenye mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Luton Town.

Mabao matatu ya Tammy Abraham yalitosha kuiwezesha Chelsea kupata ushindi wa 3-1 dhidi ya Luton, juzi Jumapili na kufuzu kucheza raundi ya tano.

Makosa ya golikipa Kepa wakati Chelsea wakiwa mbele kwa mabao 2-0, yalimfanya Jordan Clark kufunga bao la kufutia machozi.

Kepa amekuwa chaguo la pili tangu kuwasili kwa Edouard Mendy pale Stamford Bridge, lakini juzi Jumapili alipewa nafasi ya kuanza.

Werner, ambaye amefunga bao moja tu katika mechi 16 zilizopita kwenye mashindano yote, alikosa penalti dakika za majeruhi na kuendelea kuwa kwenye wakati mgumu wa kushindwa kufunga.

Tangu alipofunga bao kwenye ligi Novemba 7, mwaka jana Werner amejaribu kupiga mashuti 21, na saba pekee yakilenga lango, huku raia huyo wa Ujerumani akikosa nafasi kubwa ya kufunga.

Hata hivyo, Lampard aliwatetea wote Kepa na Werner, akisisitiza golikipa hakupaswa kulaumiwa kwa bao la Luton, huku akisema ana imani na safu yake ya ushambuliaji.

"Kepa aliokoa hatari nyingi kipindi cha pili kuhakikisha kwamba matokeo yasiwe 2-2," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni rahisi watu kumlaumu Kepa, lakini yale hayakuwa makosa yake binafsi na alicheza vizuri.

"Kwa Timo, wala sijakatishwa tamaa naye. Alicheza kwa kujituma sana. Alikuwa tishio na muunganiko wake na Tammy ulileta kitu kizuri sana."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POCHETTINO AANZA KUMVUTA MESSI PSG

**Kuwa na uwezo wa kufundishwa na kocha kutoka nchini mwako na uwezekano wa kucheza pamoja...**

**PARIS, Ufaransa**

KIUNGO wa Paris Saint-Germain, Leandro Paredes, amesema mabingwa hao wa Ligue 1 wanafanyia kazi mpango wao wa kutaka kumsajili nahodha wa Barcelona, Lionel Messi.

Messi anamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or amekuwa akihusishwa sana na PSG pamoja na miamba wa Ligi Kuu ya England, Manchester City.

Mkurugenzi wa PSG, Leonardo alibainisha kwamba kwa sasa kocha wao mpya, Mauricio Pochettino - anajaribu kumshawishi Messi, baada ya mchezaji mwenzake wa zamani pale Barca, Neymar kutoficha siri ya kutaka kucheza na raia huyo wa Argentina.

Akiwa amezungumzia kuhusu uwezekano wa Messi kutua hapo baada ya PSG kushinda 4-0 dhidi ya Montpellier Ijumaa, raia mwenzake huyo, Paredes aliliambia gazeti la Corriere dello Sport: "Ni juu ya Leo kuja klabuni, kwa sababu PSG inajaribu kumshawishi yeye.

"Kuwa na uwezo wa kufundishwa na kocha kutoka nchini mwako na uwezekano wa kucheza pamoja na Leo ni nafasi kubwa... natumaini itatokea."

Messi alikuwa benchi wakati Barcelona wakiibuka na ushindi wa 2-0 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, dhidi ya Elche, Jumapili baada ya kufungiwa mechi mbili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amefunga mabao 11 katika mechi 17 za ligi kwa Barca msimu huu, huku akiwa na mabao 14 kwenye mashindano yote.

## KWA UFUPI

**ARSENAL SAFI KWA ODEGAARD**

ARSENAL imefikia makubaliano ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, kutoka Real Madrid. ***(Mail)***

**LINGARD ARUHUSIWA KUSEPA**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, atamruhusu mshambuliaji wa Uingereza, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, kuondoka katika dirisha hili la Januari. ***(ESPN)***

**MADRID KUMSAJILI HAALAND**

REAL Madrid itaamua kupindua meza kwa kumsajili straika wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, mwenye umri wa miaka 20, ambaye anawaniwa na Chelsea na Manchester United, baada ya mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, kusema ana "furaha sana" pale Paris St-Germain. ***(Express)***

**BARCA KWA GRACIA, WIJNALDUM**

MLINZI wa Manchester City, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 20, na kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum, 30, ambao wote mikataba yao inamalizika mwishoni mwa msimu huu, wanawaniwa na Barcelona. ***(Mirror)***

**NEWCASTLE YATEUA KOCHA**

NEWCASTLE inapanga kuthibitisha kumteua Graeme Jones kama kocha wa kumsaidia Steve Bruce. ***(Telegraph)***

**DE BEEK KUBAKI UNITED**

KIUNGO wa Manchester United, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 23, yupo tayari kubaki pale Old Trafford licha ya kutopata nafasi ya kucheza, baada ya kutua hapo kwa pauni milioni 40. ***(Times)***

**GILMOUR KUONDOKA CHELSEA**

KIUNGO wa Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 19, anaweza kuondoka Chelsea kwa mkopo mwezi huu, licha ya kuanza kwenye mchezo wa Kombe la FA wa ushindi dhidi ya Luton Town, kwa mujibu wa kocha, Frank Lampard. ***(Mail)***

**MODRIC NA MKATABA MPYA**

MKURUGENZI wa Real Madrid, Emilio Butragueno amethibitisha kwamba, kiungo wa Croatia, Luka Modric mwenye umri wa miaka 35, atasaini mkataba klabuni hapo. ***(Marca)***

**KLOPP AMTAKA ALABA**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp ameiomba bodi ya klabu hiyo kutoacha nafasi ya kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, wakati atakapokuwa huru sokoni kipindi cha majira ya joto. ***(Don Balon)***

**DOKU AITAKI LIVERPOOL**

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 18, Jeremy Doku, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool, amesema amechagua kujiunga na Rennes ya Ufaransa. ***(Het Nieuwsblad, via Liverpool Echo)***

**TOSUN NA HATIMA EVERTON**

MAJALIWA ya kocha wa Uturuki, Cenk Tosun pale Everton yapo shakani baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, kuachwa kwenye kikosi hicho kilichocheza na Sheffield Wednesday kwenye mchezo wa Kombe la FA, Jumapili. ***(Liverpool Echo)***

HABARI MICHEZO

# DIDIER ATAMALIZA WATUKUTU NIDHAMU SIMBA - HITIMANA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thiery Hitimana, amesema anamfahamu vizuri Kocha Mkuu mpya wa Simba, Mfaransa Didier Gomes Da Raso, huku akimwelezea kuwa ni mtu ambaye hana uvumilivu kwa mchezaji anayeonyesha utovu wa nidhamu.

Simba juzi ilimtangaza Didier kuwa kocha mkuu akirithi mikoba ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck aliyeachia ngazi baada ya kuipeleka timu hiyo hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema Didier aliwahi kuwa bosi wake kipindi akiifundisha Rayon Sports ya Rwanda, hivyo anamfahamu vizuri utendaji wake wa kazi huku akimwelezea kuwa ni mwalimu mwenye misimamo mikali hasa lipokuja suala la nidhamu.

Alisema kocha huyo anapenda kufanya kazi kwa uweledi mkubwa na hawezi kumvumilia mchezaji yeyote kwa suala la utovu wa nidhamu (haangali jina wala umuhimu wake ndani ya kikosi) kwa kuwa yupo ambaye ataonyesha nidhamu mbovu akiamini ni adui namba moja anayekwamisha mafanikio ya klabu.

Hivi karibuni, Simba ilimsimamisha mchezaji wake tegemeo Jonas Mkude kutokana na kile kilichodaiwa ni utovu wa nidhamu na kukosa mechi mbalimbali za ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mechi dhidi ya FC Platinum kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Simba wamepata mtu sahihi wa kufikia malengo yao kwani nimefanya kazi na Didier, namfahamu ni kocha anayewajua vizuri wachezaji wa Afrika, hana uoga kwa mchezaji ambaye atakuwa anaenda kinyume cha mipango yake katika kufanikisha wanafikia malengo yanayotarajiwa.

"Falsafa yake ya kufundisha soka inaendana na Simba, anapenda sana kucheza na mfumo anaotumia, inategemea na wachezaji ambao atawakuta ndani ya timu hiyo, Simba watarajie mazuri kutoka kwa kocha huyo, viongozi na mashabiki wanatakiwa kumsapoti katika majukumu yake," alisema Hitimana.

Alisema kulingana na uwezo wa kocha huyo na kuwa na mbinu nyingi na jinsi ubora wa kikosi cha timu hiyo kilivyo bora, wachezaji wakiwa makini kufuata kile wanachofundishwa ana imani Simba itafanikiwa katika malengo yao ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hitimana alisema maslahi na ofa ambazo zinakwenda mezani kwa Didier ni sababu kubwa ambayo inamfanya aondoke na kuvunja mkataba mapema kabla ya muda wake kumalizika katika klabu mbalimbali alizozifundisha.

"Kukaa muda mfupi kwa timu alizotoka kwa sababu ya ofa nzuri zinazomfikia, ukiangalia kama hii ya mwisho ameondoka El Marreikh ya Sudan baada ya Simba kuweka dau kubwa na kufanikiwa kupata huduma yake," alisema Hitimana.

KIJAMII ZAIDI...




Kiungo wa Klabu ya Yanga, Mkongomani Mukoko Tonombe, akiwa amebeba mtoto baada ya kutoa msaada wa vitu mbalimbali juzi katika Kituo cha Watoto Yatima cha Maunga Centre kilichopo Kinondoni Mkwajuni jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Jackson Group Sport, WBF kuwanoa waamuzi wa ngumi, majaji Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Jackson Group Sport kwa kushirikiana na Shirikisho la Ngumi la Dunia (WBF), limeandaa semina ya siku moja kwa waamuzi na majaji wa Tanzania ili kuwawezesha kujua sheria mbalimbali.

Semina hiyo itafanyika leo kwenye hoteli ya Onomo jijini Dar es Salaam na kushirikisha washiriki 20 kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa.

Twissa alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa, Rais wa WBF, Howard Goldberg, ataendesha semina hiyo ambayo ni moja ya mikakati ya kampuni yao kuinua mchezo wa ngumi za kulipwa nchini.

Alisema semina hii ni jambo lao la pili tangu kuanza kuandaa ngumi za kulipwa nchini na ni moja ya mkakati wao wa kuhamasisha maendeleo ya mchezo huo kulekea pambano lao la Ijumaa kwenye Ukumbi wa Next Door Arena ambapo bondia Ibrahim Class atapambana na Dennis Mwale wa Malawi kuwania mkanda wa mabara wa uzito wa Super Feather wa WBF.

Twissa alisema Goldberg ana uzoefu wa miaka zaidi ya 40 kwenye masuala ya ngumi za kulipwa duniani na ameweza kuendesha semina kama hizo kwa nchi zaidi ya 15 pamoja na Ghana, Afrika Kusini, Misri, Gabon na Zimbabwe kwa upande wa Afrika.

"Wakati tunaendelea kuinua viwango vya mabondia nchini, tumeona pia kuongezea uwezo wa waamuzi na majaji ili kuweza kufanya kazi yao vizuri. Mara kadhaa nimesema kuwa tunachokisema ndicho tunakifanya na hii ni moja ya majukumu yetu," alisema Twissa.

## Job akabidhiwa 5 ya Yondani Yanga

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Mabingwa wa Kombe la Mapinduzi, Yanga wakianza rasmi mazoezi jana jijini Dar es Salaam, mchezaji mpya wa kikosi hicho, Dickson Job, amekabidhiwa rasmi jezi namba tano iliyokuwa ikivaliwa na beki wa zamani wa timu hiyo, Kelvin Yondani.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alisema mchezaji huyo aliyesajiliwa kutoka Mtibwa Sugar aliomba apewe jezi yenye namba tano kwa sababu wakati anaanza kucheza soka, alikuwa anamhusudu sana Yondani, hivyo ameamua kumuenzi klabuni hapo.

"Wakati anaanza kucheza soka, mchezaji aliyekuwa anamvutia mno ni Kelvin Yondani, kwa hiyo aliomba wakati tumemsajili kuwa anataka avae jezi namba tano kwa sababu ya kumuenzi, unajua Kelvin alikuwa hapa Yanga na kwa bahati nzuri Job aliyekuwa akiiga uchezaji wake naye amekuja Yanga, hivyo tumeona ni vizuri tumpatie jezi yenye namba hiyo," alisema Bumbuli.


Job, ni mmoja wa wachezaji waliosajiliwa na Yanga kwenye kipindi cha dirisha dogo.

Kuhusu mazoezi, Bumbuli alisema kuwa kikosi cha Yanga kilitarajiwa kuanza mazoezi jana, huku baadhi ya wachezaji tayari wakiwa wameshawasili.

**"Job amewasili na rafiki yake Kibwana Shomari wote kutoka Morogoro, nahodha wa kikosi Lamine Moro yeye amekuwa mtu wa kwanza kuwasili na kuonyesha mfano kwa wenzake na wengine wengi wameshawasili, wengine tunawategemea kuwasili wakati wowote, kama vile mchezaji wetu mpya Fiston Abdulrazack, kama unavyojua kuwa wachezaji wetu wengine wako kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, hao bado," alisema msemaji huyo.**

Yanga ambayo imemsajili Job katika usajili wa dirisha dogo lililofungwa Januari 15, mwaka huu, akitokea Mtibwa Sugar, iliwapa mapumziko wachezaji wake baada ya kutwaa Kombe la Mapinduzi mjini Zanzibar hivi karibuni kwa kuichapa Simba kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya suluhu ya bila kufungana ndani ya dakika 90.

Michezo
Jumanne Januari 26, 2021
Nipashe



POCHETTINO AANZA KUMVUTA MESSI PSG HABARI UK 22

ACHENI WAJE...



Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes Da Rosa (mwenye bukta nyeusi), akiwa na kikosi chake mazoezini akikiandaa kwa ajili ya michuano ya Simba Super Cup itakayoanza kesho ikishirikisha timu zingine mbili kutoka nje, TP Mazembe ya DR Congo na Al Hilal ya Sudan ambazo zote zinashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika. **MPIGAPICHA WETU**

## NYONI AIKOSA GUINEA SASA AREJESHWA DAR

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kesho ikishuka katika Uwanja wa Reunification/Douala nchini Cameroon kuvaana na Guinea kwenye mechi yake ya mwisho ya Kundi D ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itaendelea kumkosa beki wake mkongwe, Erasto Nyoni, imeelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Cliford Ndimbo, kutoka Cameroon jana, ilieleza kuwa jopo la madaktari limemruhusu Nyoni kurejea nyumbani kuendelea na matibabu zaidi.

"Mchezaji Erasto Nyoni, amepewa ruhusa ya kuondoka kwenye Kambi ya Taifa Stars, amerudi nyumbani kuendelea na matibabu baada ya kushauriwa na jopo la madaktari wa timu," ilieleza taarifa hiyo.

Katika mechi hiyo itakayopigwa majira ya saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, Stars inahitaji ushindi ili kutinga hatua ya robo fainali huku Guinea yenyewe sare yoyote ikiivusha hatua hiyo kutokana na kuongoza kundi hilo ikiwa na pointi nne sawa na Zambia ambayo nayo itashuka dimbani muda huo dhidi ya waburuza mkia wa kundi lao, Namibia.

# TP MAZEMBE NA MAJEMBE YOTE WAJA KUIVAA SIMBA

## ●●●Simba Super Cup kunoga, Jembe lingine kutoka Nigeria latua Msimbazi, Al Hilal nao waleta nyota wanaoitesa Al-Merrikh kule Sudan huku...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa zamani wa Afrika, TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Al Hilal ya Sudan zinatarajiwa kuwasili nchini leo zikiwa na 'majembe' yao ya vikosi vya kwanza kwa ajili ya kushiriki mashindano maalum ya Simba Super Cup yatakayoanza kesho jijini Dar es Salam.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema maandalizi ya mashindano hayo ya kwanza yamekamilika na wageni wao watakuja wakiwa na nyota wao muhimu wa kikosi cha kwanza kwa kila moja ikiwa na lengo la kufanya vizuri katika michuano hiyo.

Barbara alisema Simba pamoja na timu hizo mbili zimejiandaa kuonyesha burudani safi pamoja na kujiimarisha kuelekea mechi za hatua ya makundi kupitia mashindano hayo.

"Timu zote mbili zinawasili kesho (leo), TP Mazembe inakuja na mastaa wake wote muhimu kama nyota Kalaba (Rainford), tunatarajia mashindano haya yatatusaidia kiufundi na kwetu kocha atapata nafasi ya kuwaona wachezaji wake na kutengeneza mfumo atakaokuwa anautumia," alisema Barbara.

Wachezaji wa TP Mazembe ambao wametangazwa kuwa watakuwamo katika kikosi hicho mbali na Kalaba ni; Sylvain Gbohou, Patou Kabangu, Moukoro Bosso, Mputu Mabi Tresor, Thomas Ulimwengu, Moustapha Kouyate, Koffi Kouyate, Bakula Ulonde na Martial Zembe Ikoung.

Wengine ni Mayombo Etienne, Ochaya Benson, Mwape Tandi, Kabaso Chngo, Okito Kazadi Nicolas, Gmasengo Yumba Godet, Bossou Nzali Adam, Kisangala Boba, Sudi Bibonge, Tshibangu Isaac, Joel Freddy Kaougi, Bedi Guy Stephane, Binemo Madi Le Beau na Arsene Zola Kiaku.

Kuhusu michuano hiyo ya Simba Super Cup, Barbara aliongeza kuwa itakuwa ya kila mwaka na klabu hiyo itaendelea kuitafutia muda sahihi wa kufanyika ili iwe bora zaidi kiufundi kwa timu zote zitakazoshiriki.

"Kwa mfano mwaka huu tulitamani tuiweka Namungo kwa sababu nao wanashiriki mashindano ya kimataifa, lakini muda uliopo ni mdogo, nao ingewasaidia kuwaimarisha na huko mbele tunafikiria pia kuwaalika Yanga, tutawaandikia barua rasmi ya kuwajulisha," Barbara alisema.

Aliongeza kanuni za mashindano hayo zitatangazwa leo baada ya kufanyiwa kazi na Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na wanawashukuru wageni wao TP Mazembe na Al Hilal kwa kuthibitisha kushiriki michuano hiyo.

Mechi ya kwanza ya ufunguzi ya michuano hii itachezwa kesho kati ya wenyeji Simba dhidi ya Al Hilal na Januari 29, mwaka huu TP Mazembe watawakabili Wasudan hao na mchezo wa mwisho utawakutanisha Simba dhidi ya Mazembe Januari 31, mwaka huu.

Aidha, Barbara alisema baada ya michuano hiyo Simba itasafiri kuelekea jijini Dodoma tayari kwa ajili ya mechi yao ya kiporo cha Ligi Kuu Bara dhidi ya Dodoma Jiji itakayopigwa Februari 4, kabla ya siku tatu baadaye kucheza kiporo kingine katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Katika hatua nyingine klabu ya Simba jana imemtambulisha straika wake mpya, Mnigeria Junior Lokosa.

Katika ukurasa wake wa kijamii, Simba imesema lengo kuu la kumsajili mchezaji huyo ni kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini lengo mama likiwa ni kutwaa Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho, huku ikimwelezea kuwa ni straika hatari, ambaye aliwahi kuichezea timu ya Esperance ya Tunisia na ataanza kuonekana kwenye michuano ya Simba Super Cup.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002